# ATHARI ZA KIFONOLOJIA ZA LAHAJA YA KIAMU NA KITIKUU KATIKA KISWAHILI SANIFU

VIRGINIA WAIRIMU GAITHUMA

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

2016

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine

______________________________ ______________________________

**Virginia Wairimu Gaithuma** **Tarehe**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa wa Chuo Kikuu cha Nairobi

______________________________ ______________________________

**Prof. Iribe Mwangi** **Tarehe**

______________________________ ______________________________

**Dkt. Prisca Jerono** **Tarehe**

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa Samuel Gaithuma na Felista Wamaitha kwa kunilea, kunipa nafasi ya kupata elimu na kunipa moyo wa kuendelea na masomo.

Vilevile naitabarukia ndugu zangu George Ndung'u, Martin Gitau na Mercy Waithera kwa kunipa moyo wa kuendelea licha ya changamoto zote katika safari yangu ya masomo.

Pia kazi hii naitabarukia mpwa wangu Claudia aliyezaliwa katika kipindi hiki cha kuandika tasnifu hii. Mungu akupe maisha marefu.

## SHUKRANI

Mwanzo kabisa namshukuru Mwenyezi mungu kwa kunijalia uhai, afya njema na kuniwezesha kuyakamilisha masomo yangu ya uzamili. Hakika kazi kama hii haiwezi kukamilika bila ya msaada wa watu wengine. Ningependa kuzitoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliochangia kwa njia moja au nyingine katika ufanisi wa utafiti huu hasa wale ambao sikuwataja.

Kwanza kabisa shukrani zangu za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Prof. Iribe Mwangi na Dkt. Prisca Jerono ambao waliniongoza vyema kutoka mwanzo hadi nilipoikamilisha kazi hii. Daima nitawashukuru na kuwatakia heri njema na baraka za Mwenyezi Mungu kwa usaidizi na uvumilivu wao.

Pia nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili walionifundisha wakiwemo Dkt. Zaja Omboga, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Evans Mbuthia, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Rayya Timammy, Dkt. Amiri Swaleh, Prof. Habwe na Dkt. Jefwa Mweri.

Vilevile nawashukuru walimu wa shule za msingi za Wiyoni, Lamu Boys, Rasini Girls na Faza boys kwa kuniruhusu kutangamana na wanafunzi wao na kupata data iliyofanikisha utafiti huu. Hali kadhalika nawashukuru Bwana Abdurahim Bakathir na Julius Kirigha ambao nwafanyikazi katika shirika la RISSEA Mombasa kwa msaada walionipa hasa katika ukusanyaji wa data yetu.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu ambao tuliabiri pamoja katika chombo hiki na kusafiri pamoja mpaka mwisho wake licha ya changamoto zote katika mwendo huu. Nao ni Sarah, Wakesho, Lily, Dorcas, Florence, Jackline, Lavaya, Alice, Tecla, Catherine, Winnie, Braicy, Eunice, Lokidor, James, Patrick, Makori, John, Risper Seraphine, Mumo na Nyakeno.

Shukrani za kipekee kwa rafiki na mwanafunzi mwenzangu Sarah Mueni kwa kukubali kuwa kiongozi wetu wa darasa. Pia namshukuru kwa kuwa pamoja nami wakati wote nilipokuwa maktabani, kuniondolea upweke na kunipa moyo wa kuendelea muda wote tulipokuwa maktabani.

Shukrani za kipekee kwa rafiki yangu Cleoph ambaye amekuwa katika mstari wa mbele kunihimiza kulenga juu masomoni kama yeye na pia kunifadhili kwa hali na mali ili kuhakikisha kuwa nimefaulu.

## ISHARA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| [ ] | Mabano ya fonetiki |
| / / | Mabano ya fonimu |
| + | Kuwa na sifa fulani |
| - | Kutokuwa na sifa fulani |
| $L_1$ | Lugha ya kwanza |
| $L_2$ | Lugha ya pili |
| $^{h}$ | Mpumuo |

## UFAFANUZI WA DHANA

| | |
|---|---|
| LUGHA YA KWANZA | Ni lugha ambayo mtoto hujifunza mara ya kwanza anapozaliwa. Ni msingi wa lugha ambapo lugha ya pili hujengeka. Pia huitwa lugha asilia au ya mama. |
| LUGHA YA PILI | Ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha yake ya kwanza. Mara nyingi hii ni lugha ambayo watu wengi hujifunza katika masomo. |
| LUGHA YA KATI | Hii ni lugha iliyo baina ya lugha ya kwanza na lugha ya lugha ya pili . Lugha hii huzalika wakati mwanafunzi anajifundisha lugha ya pili lakini hafikii kiwango cha kuwa na umilisi kamili wa lugha lengwa kama alivyo mzawa wa lugha lengwa hiyo. |

**IKISIRI**

Tasnifu hii inahusu uchanganuzi wa athari za kifonolojia za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu ambapo uchanganuzi huu unahusu kulinganisha miundo mbalimbali ya maneno katika insha za wanafunzi na kuonyesha tofauti zinazojitokeza katika maneno kutokana na lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu. Uchunguzi huu ulinuia kubainisha fonimu za lahaja ya Kiamu na Kitikuu, kuonyesha athari za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja za Kiamu na Kitikuu katika kazi andishi za wanafunzi na pia kuorodhesha fonimu za Kiswahili sanifu. Utafiti huu umetumia nadharia ya Lugha Kati hasa kwa kurejelea mifanyiko mitano ya kisaikolojia kama mihimili mikuu. Nadharia ya Lugha Kati ilitumiwa kueleza ni vipi lugha kati huzalika miongoni mwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kiamu au Kitikuu wanapojifundisha Kiswahili sanifu. Lugha wanayoizungumza baada ya juhudi za kujifunza sio Kiswahili sanifu bali ni lugha iliyo kati ya lahaja ya Kiamu na Kitikuu na Kiswahili sanifu ambayo ndio huitwa lugha kati. Utafiti huu ulitumia mbinu ya uteuzi wa sampuli ambapo wanafunzi arobaini wa darasa la saba kutoka shule nne tofauti za kimsingi katika kisiwa cha Lamu waliteuliwa na insha walizoziandika kuchunguzwa. Matokeo ya utafiti katika tasnifu hii yanadhihirisha kwamba lahaja ya Kiamu ina fonimu 35 na lahaja ya Kitikuu ina fonimu 34. Vilevile ilidhihirika kwamba kulikuwa na athari mbalimbali za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja za Kiamu na Kitikuu ambapo athari ya matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/ ilionekana kuenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambao lugha yao ya kwanza ni aidha lahaja ya Kiamu au Kitikuu. Utafiti huu vilevile ulibainisha kwamba lahaja ya Kitikuu ilikuwa na athari nyingi za kisauti na zilizo tofauti katika Kiswahili sanifu ikilinganishwa na lahaja ya Kiamu. Mwisho ilibainika kwamba lugha iliyozungumzwa na wanafunzi tuliowachunguza ambao lugha yao ya kwanza ni aidha lahaja ya Kiamu au Kitikuu wanapojifundisha Kiswahili sanifu ni lugha kati kwani lugha hiyo haikufikia kiwango cha kuitwa Kiswahili sanifu kutokana na athari mbalimbali tulizozitambua miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

**YALIYOMO**

Ungamo ........ ii
Tabaruku ........ iii
Shukrani ........ iv
Ishara na vifupisho ........ v
Ufafanuzi wa dhana ........ vi
Ikisiri ........ vii
Yaliyomo ........ viii
**SURA YA KWANZA ........ 1**
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ........ 3
1.3 Maswali ya Utafiti ........ 4
1.4 Madhumuni ya Utafiti ........ 4
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 4
1.6 Upeo na Mipaka ........ 5
1.7 Yaliyoandikwa ........ 6
1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Lahaja ........ 6
1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Kiswahili Sanifu ........ 8
1.8 Msingi wa Nadharia ........ 11
1.8.1 Nadharia ya Lugha Kati ........ 12
1.9 Mbinu za Utafiti ........ 16
1.9.1 Uteuzi wa Sampuli ........ 16
1.9.2 Mbinu za Ukusanyaji Data ........ 17
1.9.3 Mbinu za Uchanganuzi Wa Data ........ 17
1.9.4 Uwasilishaji wa Data ........ 18
**SURA YA PILI ........ 19**
**FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU, KIAMU NA KITIKUU ........ 19**
2.1 Utangulizi ........ 19
2.2 Fonimu za Kiswahili Sanifu ........ 19
2.2.1 Fonimu za konsonanti za Kiswahili Sanifu ........ 20

2.2.2 Fonimu za irabu za Kiswahili Sanifu ........ 23
2.3 Fonimu za Lahaja ya Kiamu ........ 25
2.3.1 Viyeyusho/ Nusu Irabu ........ 28
2.3.2 Fonimu za Irabu za Lahaja ya Kiamu ........ 28
2.4 Fonimu za Lahaja ya Kitikuu ........ 30
2.4.1 Viyeyuso/ Nusu Irabu ........ 32
2.4.2 Fonimu za Irabu za Lahaja ya Kitikuu ........ 33
2.5 Hitimisho ........ 34
**SURA YA TATU ........ 35**
**ATHARI ZA KISAUTI KATIKA KISWAHILI SANIFU KUTOKANA NA LAHAJA YA KIAMU ........ 35**
3.1 Utangulizi ........ 35
3.2.1 Matumizi ya /j/ badala ya /ɟ / ........ 36
3.2.2 Matumizi ya /z/ badala ya /v/ ........ 38
3.2.3 Matumizi ya /d/ badala ya /z/ ........ 39
3.2.4 Matumizi ya /t/ badala ya /tʃ/ ........ 41
3.2.5 Matumizi ya /d/ badala ya /ɟ/ ........ 42
3.2.6 Udondoshaji wa /l/ katika maneno ........ 44
3.3 Hitimisho ........ 46
**SURA YA NNE ........ 47**
**ATHARI ZA KISAUTI KATIKA KISWAHILI SANIFU KUTOKANA NA LAHAJA YA KITIKUU ........ 47**
4.1 Utangulizi ........ 47
4.2.1 Matumizi ya /tʃ/ badala ya /t/ ........ 47
4.2.2 Matumizi ya /ð/ badala ya /z/ ........ 49
4.2.3 Matumizi ya /v/ badala ya /w/ ........ 51
4.2.4 Matumizi ya /ð/ badala ya /vy/ au /v/ ........ 53
4.2.5 Matumizi ya /n/ badala ya /m/ ........ 55
4.2.6 Matumizi ya /t/ badala ya tʃ/ ........ 57
4.2.7 Matumizi ya /d/ badala ya /ɟ / ........ 59

4.2.8 Matumizi ya /n/ badala ya /ɲ/ ... 60
4.2.9 Matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/ ... 62
4.2.10 Udondoshaji wa /m/, /l/, na /j/ katika maneno ... 64
4.3 Hitimisho ... 66
**SURA YA TANO ... 68**
**MUHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 68**
**5.1 Utangulizi ... 68**
5.2 Muhtasari ... 68
5.3 Matokeo ... 69
5.4 Hitimisho ... 71
5.5 Mapendekezo ... 72
**MAREJELEO ... 73**
**VIAMBATISHI**
**KIAMBATISHI A: KIAMU**
**KIAMBATISHI B: KITIKUU**

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Katika utafiti wetu tumechunguza athari za kifonolojia za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu ambapo tulizichunguza kazi zilizoandikwa na wanafunzi. Katika utafiti huu tumezibainisha fonimu za lahaja hizi na vilevile kuonyesha mabadiliko ya kisauti yanayojitokeza katika Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu. Bakari (1982) anaeleza kuwa lahaja ya Kiamu ndiyo inachukuliwa kuwa lahaja ya kati ya makundi mawili ya lahaja. Makundi haya ya lahaja ni lahaja za kusini na lahaja za kaskazini. Mifano ya lahaja za kusini ni kama vile Kimvita, Chijomvu, Chichifundi na Kivumba. Lahaja za kaskazini ni kama vile Kitikuu na Kisiyu. Anazidi kueleza kuwa ni muhimu kutambua kuwa lahaja ya Kiamu inaundwa kutokana na baadhi ya vipengele vinavyofanana vya lahaja hizi za kusini na kaskazini. Bakari pia anaeleza kuwa lahaja ya Kiamu huzungumzwa katika sehemu za kale za kisiwa cha Lamu ambazo ni mji wa sasa wa Lamu, Shela, Matondoni, kisiwa cha Manda na mji wa Pate. Anaeleza kuwa licha ya kuwa kijiji cha Shela na Matondoni kimetengana na mji wa Lamu kwa sababu zinazotokana na mazingira ya kijiografia kama vile mikusanyiko au milima ya mchanga, kuna mahusiano mengi mno kati ya vijiji hivi na mji wa Lamu hivyo inachukuliwa kuwa lahaja ya Kiamu ndio hutumika katika mahusiano hayo.

Chiraghdin na Mnyampala (1977) wanaeleza kuwa lahaja ya Kitikuu huzungumzwa katika sehemu za kaskazini ya Lamu katika sehemu za Rasini na katika visiwa vingine na sehemu hii huendelea hadi kufikia Kismayu mji ulioko Somalia. Wanaeleza kuwa hii ndiyo sehemu yenye mahali panapoitwa Shungwaya na ambapo ndipo chimbuko la kabila za Waswahili na kabila nyingine zilizo jirani na Waswahili yaani Wapokomo, Wagiriama, Wadigo, na hata Wasegeju. Wanaeleza pia kuwa maneno mengi ya lahaja ya Kitikuu ni sawa na ya Kiswahili cha leo. Vilevile wanaeleza kuwa Kiswahili kina lahaja zifuatazo: Kiunguja, Kingozi, Kimrima, Kimgao, Kihadimu/Kitumbatu, Kipemba, Kimtang'ata, Kipate, Kisiu, Kitikuu, Chimiini/Chimbalazi, Kingazija na Kingwana. Hata hivyo utafiti wetu ulilenga Kiswahili sanifu ambayo ni lahaja iliyosanifishwa kutokana na lahaja ya Kiunguja. Katika utafiti wetu tumeangazia Kiswahili sanifu ili kubaini ni kwa jinsi ipi kinavyoathiriwa hasa kifonolojia na lahaja za Kiamu na Kitikuu hasa kwa kuangazia kazi zilizoandikwa na wanafunzi.

Kiswahili sanifu kilibuniwa baada ya shughuli ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili kukamilika. Shughuli hii ya usanifishaji ilinuia kusuluhisha mgogoro uliokuwepo miongoni mwa waliopendelea kutumiwa kwa aidha lahaja ya Kimvita au Kiunguja katika shughuli za kibiashara, elimu na utawala. Chiraghdin na Mnyampala (1977) wanaeleza kuwa mnamo mwaka wa 1927, haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili ilikuwa imeongezeka. Katika mwaka wa 1928, mkutano wa wakilishi wa Kenya, Tanganyika, Uganda na Unguja ulifanywa Mombasa. Mkutano huu ulihudhuriwa na profesa Meinhof wa International Institute of African Languages and Cultures. Katika mkutano huu, shauri la kutumia lahaja ya Kiunguja badala ya Kimvita lilitiliwa mkazo. Mnamo tarehe mosi Januari 1930, kulibuniwa baraza lililoitwa Inter-Territorial Language Committee ili lihusike na usanifishaji wa Kiswahili. Mojawapo ya jukumu muhimu la baraza hili lilikuwa ni kuchagua lahaja ambayo ingetumiwa kama msingi wa usanifishaji kwa sababu kulikuwa na mgogoro kati ya waliopendelea Kimvita kama vile Ludwig Krapf na waliopendelea Kiunguja kama vile Bishop Steere. Kwa sababu ya ushawishi wa kiutawala na kibiashara, lahaja ya Kiunguja ilichaguliwa na hivyo kuitupilia mbali lahaja ya Kimvita ingawa lahaja ya Kimvita ilikuwa na historia ndefu hasa katika kazi zilizoandikwa ikilinganishwa na lahaja ya Kiunguja iliyopewa hadhi ya Kiswahili sanifu. Historia hii ya usanifishaji wa Kiswahili ina umuhimu katika utafiti wetu kwani inatuelezea kwa kina asili ya Kiswahili sanifu ni ipi ambayo ndio lugha tunayoichunguza katika utafiti wetu.

Maoni yetu ni kuwa Kiswahili ni lugha yenye majukumu mengi nchini Kenya kwani hutumika kama chombo cha mawasiliano na utangamano katika jamii zetu. Kwa mfano, hutumika kama lugha ya taifa ambayo huzungumzwa na raia wa makabila tofauti tofauti hivyo huwaunganisha watu hawa pamoja kwani huwawezesha kuwa na mawasiliano yenye maelewano. Vilevile Kiswahili kimepandishwa hadhi na kupewa jukumu la kuwa lugha rasmi kupitia kwa katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Hivyo Kiswahili kimekubalika kutumika katika mazingira au shughuli rasmi nchini kama vile ofisini, bungeni, biasharani na katika sekta ya elimu. Aidha Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na shule za upili ili kuwafundisha watu wote kuweza kukifahamu ili kuendeleza mawasiliano na utangamano nchini mwetu. Kiswahili vilevile hutumiwa katika kuimarisha uchumi wa nchi mbalimbali kwani husaidia katika kufanikisha biashara kwa sababu ni rahisi kueleweka na wengi. Hivyo tuling'amua kuwa ni muhimu lugha hii ya Kiswahili iweze kufanyiwa utafiti zaidi ili mambo mengi yaweze kuibuliwa na watafiti

mbalimbali na hili litachangia sana katika kuifanya lugha hii kukua na kupanua mawanda ya matumizi yake ulimwenguni.

Maelezo kuhusu lugha ya Kiswahili na majukumu yake mbalimbali yametolewa na wataalam mbalimbali kama vile, Bakari (1982) anaeleza kwamba Kiswahili ndio lugha ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi zaidi ya lugha zote katika Afrika ya kati na mashariki. Anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili hutumika kama Lingua Franka katika eneo la Afrika Mashariki. Kwa sababu hiyo lugha ya Kiswahili ilipendelewa na wamisheni walioitumia kama lugha ya Bibilia ili kuweza kueneza Injili miongoni mwa waafrika walioishi katika Afrika Mashariki. Bakari anaeleza kuwa Kiswahili vilevile kilitumiwa kama nyenzo ya kufundisha kabla ya ujio wa wamisheni. Anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili huzungumzwa kama lugha ya kwanza kwa kiwango kikubwa katika pwani ya Afrika Mashariki kuanzia Mogadishu hadi kisiwa cha Komoro. Mifano ya baadhi ya nchi za Kiafrika ambapo lugha ya Kiswahili huzungumzwa ni kama vile Kenya, Uganda, Tanzania, Zaire, Rwanda, Burundi, Mozambique na Malawi. Iribemwangi na Mukhwana (2011) wametaja Kiswahili kama Lingua Franka inayotumiwa katika shughuli za mawasiliano katika maeneo ya kusini mwa Sahara barani Afrika na Afrika Mashariki mtawalia.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Wasomi kama vile Otiende (2013), Rapando (2005) na Mbula (2011) katika kazi zao wameonyesha kuwa aghalabu kuna athari za lugha ya kwanza katika matumizi ya lugha ya pili ambapo makosa yanayojitokeza katika lugha ya pili yanatokana na ile hali ya mzungumzaji kuhamisha sifa fulani za lugha ya kwanza hadi kwenye lugha ya pili. Kila lugha huwa na muundo wake, hivyo kuhamisha sheria au sifa fulani ya lugha ya kwanza hadi katika lugha ya pili itadhihirika kama makosa. Hali hii ndiyo ilitupa msukumo wa uchunguzi kuhusu athari za kifonolojia za lahaja ya Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu hasa kwa kujikita katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi wa shule ya msingi ili tuweze kubaini kama kutakuwepo na athari katika matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lahaja za Kiamu na Kitikuu kama lugha zao za kwanza .

Tunanuia kuchunguza iwapo matokeo ya utafiti wetu yatakuwa sawa au tofauti na matokeo ya tafiti za hapo awali iwapo tutachunguza wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kiswahili lakini ni wazungumzaji wa lahaja tofauti za Kiswahili za Kiamu na Kitikuu wanapojifundisha Kiswahili sanifu. Lahaja za Kiamu, Kitikuu na Kiswahili sanifu ni lahaja zilizo na uhusiano kwa kuwa zote ni lahaja za lugha ya Kiswahili tofauti na tafiti mbalimbali zilizofanywa hapo awali kama vile Mbula (2011) ambazo zilichunguza lugha mbili tofauti zisizokuwa na uhusiano wa kilahaja

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

1. Je, lahaja ya Kiamu ina fonimu zipi?
2. Je, lahaja ya Kitikuu ina fonimu zipi?
3. Kiswahili sanifu kina fonimu zipi?
4. Je, kuna athari za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kiamu katika kazi andishi za wanafunzi?
5. Je, kuna athari za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kitikuu katika kazi andishi za wanafunzi?

## 1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI

1. Kubainisha fonimu za lahaja ya Kiamu
2. Kubainisha fonimu za lahaja za Kitikuu
3. Kuorodhesha fonimu za Kiswahili sanifu
4. Kuonyesha athari za sauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kiamu katika kazi andishi za wanafunzi.
5. Kuonyesha athari za sauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kitikuu katika kazi andishi za wanafunzi.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Hamasisho kubwa kufanya utafiti huu ni kwamba Kiswahili sanifu ni lugha ambayo imepata changamoto nyingi hasa kutokana na athari za lugha ya kwanza na ushindani mkubwa kutokana na lugha nyingine zinazopewa hadhi ya juu kama vile Kiingereza. Hivyo ili tuweze kudumisha nafasi ya lugha ya Kiswahili sanifu kama lugha rasmi na lugha ya taifa, kuna haja ya kufanya

utafiti ili kubainisha athari zozote zinazoweza kuchangia udunishaji wa muundo wa lugha ya Kiswahili sanifu na vilevile kutambua mambo mageni kuhusu lugha hii ya Kiswahili kutokana na tafiti mbalimbali zitakazofanywa na hili litachangia kwa kusaidia lugha hii ya Kiswahili kukua na kuwa na mawanda mapana ya kimatumizi.

Kazi andishi mbalimbali za wanafunzi zimedhihirisha athari nyingi za kifonolojia hasa kutokana na lugha ya kwanza. Hivyo utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika kukuza uelewaji mwema wa sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu hasa miongoni mwa wanafunzi na walimu wa Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi huu yatakuwa ya manufaa kwa walimu wa Kiswahili kwani wataweza kuyarejelea ili kuweza kuibuka na mikakati mbalimbali ya kupunguza na kurekebisha baadhi ya athari za lugha ya kwanza katika kazi andishi za wanafunzi hasa kwa kuzingatia lahaja za Kiamu na Kitikuu. Hili litakuwa na manufaa katika sekta ya elimu kwani litachangia kuboresha matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili hasa katika karatasi zote zinazotahiniwa kwani hakutakuwa na makosa mengi ya kisarufi yakidhihirika katika kazi za wanafunzi.

### 1.6 UPEO NA MIPAKA

Katika utafiti huu, tumeshughulikia athari za kifonolojia za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu. Katika utafiti wetu tumejikita katika athari za kifonolojia na kuonyesha mabadiliko ya sauti ya lahaja hizi katika Kiswahili sanifu. Katika kufanya hivyo, tumetumia insha za wanafunzi arobaini walio katika darasa la saba kutoka shule nne zilizo katika maeneo tofauti ya kisiwa cha Lamu kama vile eneo la kaskazini, eneo la mjini wa sasa wa Lamu . Tumeteua wanafunzi wa darasa la saba kwa sababu kulingana na maoni yetu ni kwamba wanafunzi hawa hawajaathiriwa sana na walimu wao kuandika insha zao pasipo kutumia lahaja zao. Walimu huwahimiza na kuwalazimisha wanafunzi katika darasa la nane kuandika insha zao kwa kutumia Kiswahili sanifu kama njia mojawapo ya matayarisho kabambe ya kufanya mtihani wa kitaifa wa somo la Kiswahili hivyo iwapo tungeteua wanafunzi wa darasa la nane, tulikadiria kuwa hatungeweza kupata matokeo ambayo yangeakisi madhumuni yetu ya utafiti. Tumetumia sampuli ya uteuzi wa hiari ya watoto arobaini ambao ni wazungumzaji wa lahaja hizi kutoka shule nne tofauti zilizo katika pande tofauti za kisiwa cha Lamu ambapo tumeteua wanafunzi kumi kutoka kila shule tulizozichagua na ambao ni wazungumzaji wa aidha lahaja za Kiamu au

Kitikuu. Nadharia tutakayoitumia katika utafiti wetu ni nadharia ya Lugha Kati iliyoasisiwa na Selinker mnamo mwaka wa 1972. Katika utafiti huu tumetumia mifanyiko mitano ya kisaikolojia inayobainishwa katika nadharia hii kama mihimili yetu.

## 1.7 YALIYOANDIKWA

Kuna mengi yameandikwa kuhusu jinsi lugha nyingi zinavyoathiri Kiswahili sanifu. Hata hivyo ikumbukwe kuwa kila lugha ina muundo na sifa zake kwa hivyo kila lugha huathiri Kiswahili sanifu kwa njia yake ya kipekee. Katika kujadili yaliyoandikwa tumeigawanya kazi hii katika sehemu mbili ambazo ni yaliyoandikwa kuhusu lahaja na yaliyoandikwa kuhusu Kiswahili sanifu.

### 1.7.1 YALIYOANDIKWA KUHUSU LAHAJA

Kazi ya Polome (1967) imetusaidia sana katika kuelewa sifa za lahaja za Kiamu na Kitikuu. Vilevile kazi hii imetusaidia kuelewa fonimu za Kiswahili sanifu na uainishaji wa fonimu hizo. Hivyo kazi hii imeuwekea utafiti wetu msingi kwani imetusaidia katika kubainisha fonimu za Kiswahili sanifu na kueleza sifa za lahaja ya Kiamu na Kitikuu. Hata hivyo kazi hii haikubainisha fonimu za lahaja za Kiamu na Kitikuu hivyo utafiti wetu umejaribu kujaza upungufu huu kwa kujaribu kuzibainisha fonimu za lahaja hizi na hili linaufanya utafiti wetu kuwa tofauti na kazi hii.

Kutokana na kazi ya Mutahi (1977) tumepata mwongozo wa jinsi tutakavyoainisha fonimu za lahaja ya Kiamu na Kitikuu kwani alishughulikia mabadiliko ya sauti na uainishaji katika makundi wa lahaja za kusini mwa Mlima Kenya ambazo ni Kiembu, Kimbeere, Kigichugu, Kindia, Kimathira, lahaja ya kaskazini na lahaja ya kusini. Kazi hii ilielezea kila mojawapo ya lahaja hizi na sehemu zinakozungumzwa. Vilevile kazi hii imetuongoza kwa kutuonyesha jinsi tutakavyolinganisha kifonolojia lahaja za Kiamu na Kitikuu na Kiswahili sanifu kwa sababu Mutahi alichunguza na kuonyesha jinsi lahaja hizi saba zinavyolingana na kutofautiana kifonolojia. Hata hivyo utafiti wetu unatofautiana na kazi hii kwani tumechunguza athari za lahaja ya Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu wala sio lahaja za sehemu ya kusini mwa Mlima Kenya kama utafiti huo ulivyochunguza.

Utafiti wetu umepata mchango mkubwa mno kuhusu maelezo ya lahaja mbalimbali za Kiswahili na zinakozungumzwa kutokana na kazi ya Chiraghdin na Mnyampala (1977) kwani wameelezea lahaja mbalimbali za Kiswahili kama vile Kingozi, Kiunguja, Kimrima, Kimgao, Kihadimu/Kitumbatu, Kipemba, Kimtang'ata, Kipate, Kisiu, Kitikuu, Chimiini, Kingazija na Kingwana. Kazi hii ina upungufu wa kimaelezo kwani haikuelezea kwa kina zaidi kuhusu lahaja hizi za Kiswahili. Hivyo utafiti wetu unanuia kuujaza upungufu huu kwa kuzichunguza lahaja hizi kwa kina zaidi kwa kubainisha fonimu za lahaja za Kiamu na Kitikuu na kuzilinganisha na fonimu za Kiswahili sanifu na kuonyesha mabadiliko ya kisauti. Aidha utafiti wetu unatofautiana na kazi hii kwani tumezichunguza lahaja za Kiamu na Kitikuu kwa kubainisha fonimu zake na kisha kuonyesha zinavyotofautiana na fonimu za Kiswahili sanifu.

Tumepata mwongozo wa jinsi tutakavyoonyesha mabadiliko ya kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kiamu na Kitikuu kwa kuitathmini kazi ya Maundu (1980). Katika kazi yake aliangazia kuhusu mabadiliko makuu ya sauti za konsonanti za lugha ya Kikamba. Alionyesha mabadiliko hayo katika lahaja nne za Kikamba ambazo ni Kikilungu, lahaja ya Kikamba sanifu, lahaja ya kaskazini mwa Kitui na lahaja ya kati mwa Kitui. Hata hivyo utafiti huu unatofautiana na utafiti wetu kwani ulichunguza mabadiliko ya sauti ya lahaja za Kikamba ilhali utafiti wetu umechunguza mabadiliko ya kisauti ya lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu kwenye maandishi.

Utafiti wetu umepata mchango mkubwa kuhusu maelezo ya historia ya lahaja ya Kiamu na Kitikuu na lugha ya Kiswahili kutoka kwa kazi yake Bakari (1982). Bakari alichanganua mofofonolojia ya lahaja saba za Kiswahili za Kenya zinazozungumzwa katika pwani ya Kenya. Alijaribu kuonyesha kwa njia yenye utaratibu mifanyiko ya kimofofonolojia katika kila mojawapo ya lahaja hizi ili kuwezesha kuibuka na njia ya kisayansi ya kubainisha au kutofautisha lahaja hizi. Kazi hii imetusaidia katika kuonyesha jinsi lahaja za Kiamu na Kitikuu zinavyotofautiana kwa kuzingatia mabadiliko ya kisauti yanayotokana na mifanyiko ya kifonolojia. Utafiti wetu unatofautiana na wa Bakari kwa sababu tumechunguza athari za kifonolojia za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu ilhali utafiti wake ulichunguza mofofonolojia ya lahaja za Kiswahili za Kenya. Udhaifu wa kazi hii ni kuwa alijikita katika uchunguzi wa lahaja pekee na hakutoa ulinganisho wa lahaja hizi na lahaja nyingine ambayo

ndio iliyoteuliwa kutumika. Tumejaribu kuujaza upungufu huu kwa kulinganisha lahaja za Kiamu na Kitikuu na Kiswahili sanifu na kubainisha fonimu mbalimbali za lahaja hizi na kuonyesha mabadiliko ya kisauti yanayojitokeza.

Kutokana na kazi ya Otiende (2013) tumepata mchango mkubwa katika utafiti wetu kuhusu uainishaji wetu wa fonimu za Kiswahili sanifu na vilevile kazi hii imetuongoza katika jinsi tutakavyolinganisha Kiswahili sanifu na lahaja za Kiamu na Kitikuu kwani katika utafiti wake alichunguza kuhusu athari za kimofofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili. Katika kazi yake ameziainisha fonimu za Kiswahili sanifu katika makundi matatu; fonimu za irabu, za nusu irabu na za konsonanti  hili limetusaidia katika uainishaji wetu wa fonimu za Kiswahili sanifu. Vilevile kwa kila mojawapo ya aina hizi za fonimu alizitolea mifano na hata kuziwasilisha katika maumbo tofauti hivyo kazi hii imetufaidi sana katika kuziainisha fonimu za Kiswahili sanifu katika utafiti wetu. Hata hivyo utafiti huu unatofautiana na utafiti wetu kwani unachunguza athari za kimofofonolojia ilhali utafiti wetu umechunguza athari za kifonolojia za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu.

### 1.7.2 YALIYOANDIKWA KUHUSU KISWAHILI SANIFU

Utafiti wetu umepata mchango mkubwa katika kuelezea fonolojia ya Kiswahili sanifu kutoka kwa kazi ya Chepkwony (1993). Katika kazi yake alichunguza kuhusu fonolojia ya Kiswahili na Kinandi na kuonyesha jinsi lugha hizi zinavyotofautiana kifonolojia na kimofolojia. Hivyo imetuongoza katika kuziorodhesha fonimu za Kiswahili sanifu kama mojawapo ya madhumuni katika utafiti wetu. Kazi hii pia imetuongoza katika jinsi ya kuzibainisha athari za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu kwani Chepkwony alichunguza matatizo au makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kiswahili wenye asili ya Kinandi na kuelezea sababu ya makosa hayo. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wetu kwa sababu ulishughulikia lugha mbili zilizo na sifa tofauti kabisa yaani Kinandi( Kinailoti)na Kiswahii(Kibantu) ilhali katika utafiti wetu tumechunguza lahaja za Kiamu na Kitikuu ambazo ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili hivyo lugha hizi zinazochunguzwa zina uhusiano mkubwa mno.

Kazi ya Mgullu (1999) imekuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu kwani imetusaidia katika kuelezea fonolojia ya Kiswahili sanifu hasa kwa kuonyesha fonimu za lugha ya Kiswahili.

Kazi hii imejadili kwa kina zaidi kuhusu fonolojia na mofolojia ya Kiswahili sanifu hivyo imetufaa sana katika sura ya pili ya utafiti wetu. Hata hivyo utafiti wetu unatofautiana na kazi hii kwani tumeshughulika na uchunguzi wa lahaja za Kiamu na Kitikuu na wala sio Kiswahili sanifu pekee kama ilivyo katika kazi yake Mgullu.

Utafiti wetu umepata mchango mkubwa kutoka kwa kazi ya Kihore na wenzake (2001) kwani tumepata maelezo kuhusu fonolojia ya Kiswahili sanifu ambapo wameelezea kuhusu sauti za Kiswahili sanifu na kuziandika kifonetiki na vilevile kuchora kielelezo cha jedwali la aina za konsonati na irabu za Kiswahili sanifu hivyo kazi hii imetufaa zaidi katika sura ya pili ya utafiti wetu. Kazi hii inatofautiana na utafiti wetu kwa sababu utafiti wetu haujashughulikia lugha ya Kiswahili sanifu pekee bali pia ulihusisha uchunguzi wa lahaja za Kiamu na Kitikuu ambapo tumezibainisha fonimu za lahaja hizi na kuonyesha mabadiliko ya sauti yanayojitokeza katika Kiswahili sanifu kutokana na athari za lahaja hizi.

Mchango mwingine katika utafiti wetu kuhusu fonolojia ya Kiswahili tumeupata katika kazi ya Habwe na karanja (2004) kazi hii imeeleza kuhusu fonimu mbali mbali za Kiswahili na kuziainisha katika makundi. Hivyo maelezo haya yametufaa katika utafiti wetu katika kuziorodhesha fonimu za Kiswahili sanifu. Aidha utafiti wetu unatofautiana na kazi hii kwani haujajikita katika kuchunguza Kiswahili sanifu pekee bali pia tumechunguza fonimu za lahaja za Kiamu na Kitikuu. Utafiti wetu umejaribu kujaza upungufu wa kazi hii kwa kuchunguza pia fonolojia ya lahaja za Kiswahili (Kiamu na Kitikuu).

Kazi ya Massamba na wenzake (2004) imetufaa katika utafiti wetu kwani imejadili kuhusu masuala ya kijumla ya fonolojia ya Kiswahili sanifu ambapo wamezibainisha fonimu mbalimbali za Kiswahili hivyo maelezo hayo yametufaa katika kujadili kwetu kuhusu fonimu za Kiswahili. Kazi hii inatofautiana na kazi yetu kwani ilishughulikia tu uchunguzi wa Kiswahili sanifu ilhali tumeshughulikia Kiswahili sanifu na vilevile kuchunguza fonoloija ya lahaja mbili za Kiswahili ambazo ni Kiamu na Kitikuu.

Utafiti wake Rapando (2005) umekuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu hasa kutokana na matokeo ya utafiti wake. Rapando alichunguza makosa ya kimofo-sintaksia yanavyojitokeza

katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi. Katika utafiti wake alitambua kuwa baadhi ya makosa hayo yalisababishwa na lugha ya kwanza na pia kutokana na ujumlishaji mno miongoni mwa wanafunzi. Hivyo matokeo haya yatatufaa kwani baadhi ya sababu walizozitambua kusababisha makosa hayo ni kama vile athari ya lugha ya kwanza na ujumlishaji mno ni miongoni mwa mihimili ya nadharia ya lugha kati tuliyotumia katika utafiti wetu kuchunguza athari za kifonolojia za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu. Utafiti wetu umekuwa tofauti na kazi hii kwa sababu haujachunguza Kiswahili sanifu pekee bali tumechunguza hata lahaja za Kiswahili ambazo ni Kiamu na Kitikuu. Vilevile katika ukusanyaji data, Rapando alitumia wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi ilhali katika utafiti wetu tumetumia wanafunzi wa shule za msingi jijini Lamu.

Katika kazi ya Njogu na wenzake (2006) tumepata mchango kuhusu fonolojia ya Kiswahili sanifu kwa sababu kazi hii inachanganua fonimu za Kiswahili katika mojawapo ya sura zilizomo katika kazi hii. Tofauti iliopo kati ya kazi hii na utafiti wetu ni kuwa utafiti wetu umechunguza lugha zaidi sio Kiswahili pekee kama ilivyo kazi hii.

Tumepata mchango mkubwa kuhusu fonolojia ya Kiswahili sanifu kutoka kwa kazi ya Iribemwangi (2010) kwa sababu katika sura ya kwanza alijadili kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili na mambo ya kijumla kuhusu lugha ya Kiswahili sanifu. Vilevile kazi hii imejadili kwa kina zaidi kuhusu fonolojia ya Kiswahili sanifu katika sura ya pili. Hivyo kazi hii inauwekea utafiti wetu msingi thabiti kwani imetuongoza katika kuziorodhesha fonimu za Kiswahili sanifu. Utafiti wetu unatofautiana na kazi hii kwani kando na kuchunguza Kiswahili sanifu, utafiti wetu umechunguza lahaja ya Kiamu na Kitikuu. Kazi hii pia ilishughulikia mofofonolojia ya fonimu za Kiswahili ilhali utafiti wetu haujachunguza mofofonolojia ya fonimu za Kiswahili sanifu bali tumechunguza athari za kifonolojia.

Matokeo ya utafiti wa Mbula (2011) yamekuwa na mchango mkubwa mno katika utafiti wetu kwani alitafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kikamba wanapojifunza Kiswahili sanifu. Mbula alitambua kuwa makosa mengi yanayofanywa na wanafunzi ni ya kifonolojia na yanathibitisha kuwepo kwa lugha kati badala ya kuwepo kwa lugha lengwa ambayo ni Kiswahili sanifu. Pia alitambua kuwa wanafunzi ambao

lugha yao ya kwanza ni Kikamba na wanaojifundisha Kiswahili sanifu hufanya makosa kwa sababu ya kuhamisha mifumo ya kiisimu ya lugha yao ya kwanza (Kikamba) na kulazimisha mifumo hiyo kuwepo katika Kiswahili sanifu hivyo badala ya kuibuka na Kiswahili sanifu wanaishia kuibuka na lugha kati. Hivyo kazi hii imetufaa zaidi katika utafiti wetu kwani alitumia nadharia ya Lugha Kati ambayo ndiyo nadharia tuliyoitumia katika utafiti wetu. Zaidi ya hilo, utafiti huu unaelezea namna ambavyo wanafunzi wanaojifundisha lugha ya pili huathiriwa na ujuzi wa lugha ya kwanza hivyo utafiti huu ulitupa ari ya kuchunguza iwapo tungepata matokeo sawa iwapo tungechunguza wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kiswahili lakini wanatumia lahaja mbalimbali za Kiswahili hivyo tulichunguza iwapo lahaja hizi huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu na kusababisha kuibuka kwa lugha kati ambayo katika utafiti huu ni lugha iliyo kati ya lahaja hizi na Kiswahili sanifu. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wetu kwani unachunguza miundo ya lugha ya Kikamba ilhali utafiti wetu unachunguza miundo ya Kiswahili sanifu, Kiamu na Kitikuu. Pia alichunguza makosa ya wazungumzaji ambao lugha yao ya kwanza ni Kikamba ilhali sisi tumechunguza lahaja za Kiamu na Kitikuu.

## 1.8 MSINGI WA NADHARIA

Iwapo mtu anataka kujifunza lugha ya kigeni ni kawaida kuwa atakumbana na changamoto mbalimbali za ujifundishaji hasa kuhusiana na mfumo wa sauti, msamiati na muundo wa lugha hiyo anayojifundisha. Jambo hili linaeleweka kwa sababu mwanafunzi anayejifundisha lugha hii ya kigeni amekuwa akizungumza lugha asilia yake ambayo huwa imejengeka ndani mwake kama jambo la mazoea. Mara nyingi mwanafunzi huyu huhamisha mazoea hayo kwenye lugha lengwa anayojifundisha jambo ambalo linasababisha kutokea kwa makosa. Kulingana na Rustipa (2011) nadharia ya Uchanganuzi Kinyume *(contrastive analysis)* ilioasisiwa na Fries (1945) hudai kuwa makosa haya husababishwa na elementi mbalimbali kati ya lugha asilia na lugha lengwa. Hivyo wafuasi wa nadharia hii ya Uchanganuzi Kinyume wanapendekeza kuwa walimu wafanye uchanganuzi wa kinyume kati ya lugha asilia na lugha lengwa ili kuweza kutabiri changamoto za ujifundishaji ambazo wanafunzi wa lugha watakumbana nazo. Hata hivyo sio makosa yote yaliyotabiriwa na nadharia ya Uchanganuzi Kinyume hujitokeza kuwa masuala magumu kwa wanafunzi wa lugha. Kwa upande mwingine, makosa mengi ambayo huchipuza huwa hayajatabiriwa na nadharia ya Uchanganuzi Kinyume. Udhaifu huu umechangia kuibuka

kwa nadharia ya Uchanganuzi Makosa *(error analysis)* ambayo iliasisiwa na Corder katika miaka ya 1960s.

Kwa mujibu wa Corder (1967) matokeo muhimu ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni kuwa makosa mengi ya kiuchukulizi hufanywa na wanafunzi kwa sababu ya kuwa na uchukulizi wenye matatizo kuhusu sheria za lugha lengwa. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilionyesha kuwa nadharia ya Uchanganuzi Kinyume haikuweza kutabiri kwa wingi makosa mengi ingawa mambo muhimu ya uhamishaji lugha yamejumuishwa katika uchunguzi wa uhamishaji lugha. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni uchunguzi wa aina na kiasi cha makosa ambayo hutokea hasa katika taaluma ya isimu tumizi. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilikosolewa kwa kupotosha kuhusu changamoto za ujifundishaji wa wanafunzi kwa sababu ya ujiepushaji wake wa elementi ngumu za lugha lengwa. Hili lilisababishwa kuibuliwa kwa nadharia ya Lugha Kati katika miaka ya sabini na mwanaisimu wa Kimarekani aliyeitwa Larry Selinker.

### 1.8.1 NADHARIA YA LUGHA KATI


Nadharia ya Lugha Kati inaelezea kuwa mtu anapojifundisha lugha ya pili hawezi kupata umahiri kamili au wa asilimia moja wa lugha hiyo anayojifundisha kiasi cha kuzungumza sawa na mzawa wa lugha hiyo bali lugha anayoipata mwanafunzi wa lugha hiyo huwa ni lugha iliyo kati ya lugha yake asilia na lugha lengwa anayojifundisha. Hii ni kwa sababu lugha atakayoizungumza itakuwa imepata sifa fulani hivyo kuifanya tofauti na lugha ya kwanza lakini haiwezi kufikia kiwango cha lugha lengwa kwani kuna baadhi ya vipengele vya lugha hiyo hataweza kuvipata katika ujifundishaji lugha hiyo. Kulingana na Tarone (2006) dhana hii ya lugha kati ilizalishwa na mwanaisimu wa kimarekani aliyeitwa Larry Selinker katika mwaka wa 1972. Tarone alielezea kuwa nadharia ya Lugha Kati ni mfumo wa kiisimu unaodhihirika wakati mwanafunzi wa lugha ya pili anapojaribu kuwasilisha maana katika lugha anayojifundisha. Lugha kati huonekana kuwa mfumo wa kando wa kiisimu ambao ni tofauti kabisa na lugha asilia ya mwanafunzi na lugha lengwa anayojifundisha ingawa unahusiana na lugha asilia na lugha lengwa kwa vibainishi na mielekeo ya lugha kati ya mwanafunzi. Mfumo huu wa kiisimu unajumuisha sio tu fonolojia, mofolojia na sintaksia bali pia leksia, pragmantiki na daraja mbali mbali za mazungumzo ya lugha kati.

Mfumo wa lugha kati sio mfumo wa kimofolojia na kisintaksia wa lugha asilia unaobadilishwa na msamiati wa lugha lengwa, yaani sio mfumo wa kimofolojia na kisintaksia ambao ungedhihirika iwapo mwanafunzi angejaribu kuwasilisha maana hizo katika lugha asilia yake. Vile vile sio mfumo wa lugha lengwa ambao ungedhihirika iwapo wazungumzaji asilia wa lugha lengwa wangejaribu kuwasilisha maana hizo hizo bali lugha kati hutofautiana kimfumo na lugha asilia na lugha lengwa. Ellis (1989) anaeleza kuwa nadharia ya Lugha Kati ni nadharia inayowekea msingi juhudi za watafiti juu ya upataji lugha ya pili ili kuweza kutambua daraja za maendeleo ya ujifunzaji ambazo wanafunzi wa lugha ya pili hupitia katika kujifundisha lugha ya pili kwa ufasaha au kukaribia lugha ya pili. Makosa yanayofanywa na wanafunzi wa lugha ya pili ni njia ambazo lazima zifuatwe na wote wanaojifundisha lugha kwani makosa ni thibitisho la haipothesia. Khansir (2012) akiwarejelea Tarone, E. na wenzake (1976) anaeleza kuwa wazungumzaji wa lugha ya pili kwa mara chache hufuata yale ambayo mtu angetarajia kutoka kwa wazungumzaji asilia wa lugha lengwa kuweza kuzungumza na matamshi katika lugha ya pili hayatolewi pasipokuwa na utaratibu maalum. Lugha kati inayozungumzwa aidha na watu wazima au watoto wakati wa upataji lugha ya pili sio sambamba na upataji lugha wa lugha ya kwanza. Rustipa (2011) akiwarejelea Larsen na wenzake (1992) alielezea kuwa lugha kati ni mfululizo kati ya lugha ya kwanza na lugha lengwa ambapo wanafunzi wote hupitia. Alitumia dhana ya lugha kati kurejelea aina isiyo wastani ya lugha ya kwanza au ya pili inayotumiwa kama mbinu ya mawasiliano katika makundi.

Selinker (1992) anaeleza kuwa lugha kati huundwa na mwanafunzi wa lugha ya pili ambaye hajakuwa na uwezo ulioimarika ingawa anakaribiana na lugha lengwa na kuhifadhi baadhi ya sifa za lugha ya kwanza au ujumlishaji zaidi wa kanuni za lugha lengwa katika kuzungumza au kuandika lugha lengwa na kuibuka na uvumbuzi. Kanuni za lugha kati zinaundwa kutokana na uhamishaji lugha ya kwanza, uhamishaji wa yaliyosomwa, mbinu za kufunza lugha ya pili, mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili na ujumlishaji mno wa ruwaza za lugha lengwa. Lugha kati inaweza kufikia kikomo na kukosa kuendelea kukua katika daraja za ukuaji. Huku ni kule kufikia ukomaji wa kudumu wa kutoendelea kuelekea katika lugha kati. Ukomaji huu unaweza kutokea licha ya majaribio yote katika kujifundisha.Ukomaji huu kwa lugha huhusisha vitu na miundo midogo ambayo wanafunzi wa lugha ya pili huishia kuishika na kuhifadhi katika

lugha kati yao na vipengele hivi huingizwa na kuwa za kudumu katika lugha kati. Ufuatao ni mchoro wetu tulioibuka nao kuonyesha dhana ya lugha kati.

**Kielelezo 1**




Lugha Kati

Asili: Utafiti wetu tulioufanya

Selinker anaibainisha michakato ya isimu nafsia ifuatayo kuwa ndio huunda lugha kati na michakato hii ndiyo mihimili ya nadharia hii na ndio tutakayoitumia katika utafiti wetu.

1. Uhamishaji lugha asilia.
2. Ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa.
3. Uhamishaji wa yaliyosomwa.
4. Mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili.
5. Mbinu za kufunza lugha ya pili.

**Uhamishaji lugha asilia**

Hii ni njia ambayo wachanganuzi wa nadharia ya Uchanganuzi Kinyume walikuwa wamependekeza kama njia muhimu sana katika kukuza lugha ya mwanafunzi na vilevile ina jukumu muhimu sana katika kuunda haipothesia za lugha kati ingawa hii sio mbinu pekee inayohusika, kuna ithibati tosha ya utafiti inayoonyesha kuwa mbinu hii ina jukumu muhimu sana katika kuunda miundo ya lugha kati ya wanafunzi. Selinker (1992) anadai kuwa njia ambayo hili hutokea ni kuwa wanafunzi huunda vibainishi vya lugha kati katika kujifundisha lugha ya pili ambapo wanachukulia baadhi ya vipengele kuwa sawa katika lugha asilia, lugha kati na lugha lengwa. Selinker alidai kuwa katika isimu ya kimuundo ya kikale, vitu huelezwa kwa mujibu wa mfumo wa kiisimu ambapo huwa vinajitokeza na havina maana nje ya mfumo huo. Hata hivyo katika kuunda vibainishi vya lugha kati wanafunzi wa lugha ya pili hupanua

vipengele vya kiisimu kwa kuchukulia kuwa vina maana sawa katika mifumo yote mitatu (lugha asilia, lugha kati na lugha lengwa).

**Ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa**

Hii ni mbinu ambapo mwanafunzi huonyesha ithibati ya kuwa ameshika kanuni ya kijumla ya lugha lengwa lakini hajui mipaka ya matumizi ya kanuni hiyo ni ipi na ni lini kanuni hiyo haitumiki. Makosa ya ujumlishaji mno huonyesha wazi ithibati ya kuwepo na maendeleo ya upataji lugha kwani huonyesha kuwa mwanafunzi ameshika kanuni ya lugha lengwa na vile vile huonyesha ni mambo yepi mengine ambayo mwanafunzi hajapata kujifundisha.

**Uhamishaji wa yaliyosomwa**

Hutokea wakati mwanafunzi wa lugha ya pili hutumia kanuni alizojifundisha kutoka kwa walimu au vitabu. Wakati mwingine ujifundishaji huu hufaulu kwani kanuni ya lugha kati inayozaliwa haiwezi kutofautishwa sana kutokana na kanuni ya lugha lengwa ingawa wakati mwingine makosa hutokea.

**Mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili**

Hutumiwa na mwanafunzi kusuluhisha matatizo ya kimawasiliano wakati ambapo mfumo wa lugha kati unaonekana kutokimu mahitaji yake. Katika juhudi za kuwasilisha maana wakati ambapo mwanafunzi huhisi kuwa kipengele cha kiisimu kinachohitajika hakipatikani anaweza kutumia mikakati mbali mbali ya mawasiliano ili kuwasilisha maana. Miundo na ruwaza hizi za kiisimu zinazotumiwa katika juhudi ya kuwasilisha maana zinaweza kuwa sehemu za kudumu za lugha kati ya wanafunzi.

**Mbinu za kufunza lugha ya pili**

Hutumiwa na wanafunzi katika juhudi za kushika lugha lengwa. Mojawapo ya mikakati ya ujifundishaji ni ulinganishi wa wanafunzi wa yale wanayozungumza katika lugha kati na yaliyomo katika lugha asilia na kinachochukuliwa kuwa lugha lengwa hivyo wanafunzi huishia

kuunda vibainishi vya lugha kati. Mifano ya mikakati ya ujifunzaji ni kama vile matumizi ya kumbukizi ili kukumbuka msamiati katika lugha lengwa, ukariri wa mazungumzo yaliyomo vitabuni, matumizi ya kadi za maswali na majibu. Mikakati kama hii mara nyingi hufaulu ingawa inaweza kuishia kuwa ni makosa. Orodha zilizokaririwa zinaweza kuleta mkanganyiko baina ya maneno.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

Tumeweza kupata data yetu kutokana na utafiti wa maktabani ambapo tuliweza kupata data kuhusu fonolojia ya Kiswahili sanifu, lahaja za Kiswahili na maelezo kuhusu nadharia ya Lugha Kati kutokana na vitabu, mtandao na tasnifu zilizo maktabani. Pia tulitumia utafiti wa nyanjani ambapo tulizuru mji wa Lamu na kuteua shule nne tofauti za msingi zinazopatikana katika kisiwa cha Lamu ambapo tuliweza kuteua sampuli ya wanafunzi wa darasa la saba kutoka shule hizo ambao ni wazungumzaji wa aidha lahaja za Kiamu na Kitikuu kama lugha yao ya kwanza. Ili kuyafikia malengo ya utafiti katika mipaka ya nadharia husika lazima harakati za utafiti zishughulikiwe kwa utaratibu na kwa njia mwafaka. Nadharia ya Lugha Kati ilikuwa muhimu kwetu kwani ndio imetumika kueleza kwa nini wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kiswahili lakini ni wazungumzaji wa lahaja za Kiswahili hasa lahaja za Kiamu na Kitikuu kama lugha zao za kwanza huishia kuibuka na lugha iliyo katikati ya lugha asilia na lugha lengwa yaani lugha kati wanapotumia Kiswahili sanifu.

### 1.9.1 UTEUZI WA SAMPULI

Lahaja za Kiamu na Kitikuu ni lahaja za Kiswahili zinazozunguzwa katika kisiwa cha Lamu. Tumetumia sampuli ya kubahatisha ya watoto arobaini ambao ni wazungumzaji wa lahaja hizi. Sampuli yetu tuliipata kutoka kwa shule za msingi nne zinazopatikana katika kisiwa cha Lamu. Tulitumia sampuli ya uteuzi wa hiari kuchagua shule hizi nne tulizozichunguza. Shule tulizoziteua kufanyia utafiti wetu ni shule ya msingi ya Wiyoni, Lamu Boys, Rasini Girls na Faza Boys. Sababu yetu ya kuchagua shule hizi ni kwa sababu zinapatikana katika maeneo ambamo lahaja hizi hutumika zaidi. Kwa mfano lahaja ya Kiamu hutumika zaidi katika eneo la sehemu za kale za kisiwa cha Lamu kama vile mji wa sasa wa Lamu ndiposa tukateua shule ya msingi ya Wiyoni na Lamu Boys. Lahaja ya Kitikuu hutumika sana katika sehemu za kaskazini ya Lamu ndiposa tukateua shule ya msingi ya Rasini Girls na Faza Boys. Tuliweza kubainisha ni

sauti zipi za Kiamu na Kitikuu kwa sababu mimi ni karibu ya mzungumzaji asilia wa Kiswahili sanifu hivyo tuliweza kutofautisha sauti za lahaja hizi za Kiamu na Kitikuu na zile za Kiswahili sanifu.

### 1.9.2 MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

Katika utafiti wetu tumetumia data msingi. Data msingi ni taarifa au maandishi asilia ambayo mtafiti hupata baada ya kufanya utafiti nyanjani hivyo habari hizi huwa hazijaathiriwa na vishawishi vyovyote. Mbinu tuliyoitumia katika kukusanya data katika utafiti wetu ni mbinu ya kutumia sampuli ambapo tulitumia aina mbili za sampuli ambazo ni sampuli ya uteuzi wa hiari ili kuteua shule nne tulizochunguza wanafunzi wake. Tulitumia sampuli ya kubahatisha ili kuwateua wanafunzi arobaini kutoka shule hizi nne tulizozichagua ambapo tuliteua wanafunzi wowote kumi kutoka kila mojawapo ya shule hizi ambao ni wazungumzaji wa aidha ya lahaja za Kiamu au Kitikuu. Wanafunzi tuliowahusisha katika utafiti wetu ni wa darasa la saba pekee kwa sababu wanafunzi hawa wamefundishwa kwa ukamilifu miundo ya maneno ya Kiswahili sanifu hivyo wana ufahamu wa kutosha wa kanuni zinazotawala matumizi ya Kiswahili sanifu. Wanafunzi hao waliandika insha ambazo tulizisahihisha kwa makini na kujaribu kuyaorodhesha makosa yao huku tukiyaainisha katika makundi kulingana na aina zake. Pia tulinasa baadhi ya mazungumzo ya wanafunzi ambao ni wazawa wa lahaja hizi ili kusikiliza jinsi walivyoathirika katika matumizi yao ya Kiswahili sanifu.

### 1.9.3 MBINU ZA UCHANGANUZI WA DATA

Baada ya kutoka nyanjani, tulizisoma insha hizo kwa makini na kujaribu kuzitambua athari za lahaja hizi kwa kuorodhesha maneno yote yaliyodhihirisha athari za lahaja za Kiamu na Kitikuu na kuyaandika maneno haya kwa Kiswahili sanifu ili kuonyesha tofauti kati ya maneno hayo na Kiswahili sanifu. Kisha tulionyesha mabadiliko ya sauti ya lahaja hizi katika Kiswahili sanifu kwa kuzingatia mifano ya maneno ambayo tuliyaorodhesha kutokana na insha mbalimbali za wanafunzi. Tulitumia mifanyiko ile mitano ya nadharia ya Lugha Kati tuliyoijadili hapo awali ili kuweza kuchanganua na kutambua ni mifanyiko ipi iliyoweza kusababisha mabadiliko mbalimbali ya kisauti ya lahaja hizi katika Kiswahili sanifu hasa kwa kuzingatia insha tulizokuwa tumezisoma na kuzisahihisha. Pia tuliyasikiliza mazungumzo tuliyoyanasa kwa makini na kuyadondoa maneno yanayoashiria athari hizi. Vilevile tulichora mchoro kwa kila

mojawapo ya athari tulizozitambua ili kuonyesha asilimia ya kutokea kwa athari hizo miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

### 1.9.4 UWASILISHAJI WA DATA

Data yetu imewasilishwa kwa njia ya kutumia mchoro wa mviringo wa asilimia ambapo tumeonyesha kila mojawapo ya athari za kisauti tulizozitambua kutokana na lahaja za Kiamu na Kitikuu. Sababu yetu ya kuchagua michoro ya asilimia ni kwamba ilituwezesha kuonyesha ni asilimia ngapi ya wanafunzi tuliowachunguza ambao walikuwa na athari mbalimbali tulizozitambua. Vilevile tuliweza kubainisha ni asilimia ngapi ya wanafunzi hawakuwa na athari hizo za kisauti tulizozitambua. Kutokana na michoro hii ya asilimia pia tuliweza kutambua ni athari zipi zilikuwa zimeenea zaidi au ni athari zipi hazikuenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

# SURA YA PILI

# FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU, KIAMU NA KITIKUU

## 2.1 Utangulizi

Madhumuni ya sura hii ni kuainisha fonimu za Kiswahili sanifu, fonimu za lahaja ya Kiamu na vilevile fonimu za lahaja ya Kitikuu na vilevile kuonyesha lahaja hizi zina tofauti zipi katika idadi ya sauti. Ili kuelewa mifumo ya lugha hizi kwa ukamilifu, ni vyema na muhimu kuelewa mifumo ya sauti zake. Kipengele muhimu katika uchunguzi wa fonolojia ni fonimu. Kiswahili sanifu na lahaja za Kiamu na Kitikuu ni lahaja ambazo zinaweza kuwa na sauti zinazowiana kwa sababu lahaja hizi za Kiamu na Kitikuu ni mojawapo ya lahaja za Kiswahili hivyo tunaweza kukadiria kuwa zina sifa za sauti za kimsingi zinazowiana. Hata hivyo lugha hizi haziwezi kuwa na vipengele vyote sawa vya sauti kwani hakuna lugha mbili au zaidi ambazo hufanana kikamilifu katika mifumo yake ya kisauti kama tulivyoshuhudia katika utafiti wetu ambapo tulitambua kwamba lahaja za Kiamu na Kitikuu zina sauti zilizo na mpumuo ilhali kuna madai miongoni mwa wataalam mbalimbali kwamba lugha ya Kiswahili sanifu haina sauti zilizo na sifa ya mpumuo ambao ndio mwelekeo tuliouchukua katika utafiti wetu. Tulibainisha kwamba fonimu za lahaja za Kiswahili sanifu, Kiamu na Kitikuu zimegawika katika makundi matatu ambayo ni konsonanti, irabu na viyeyusho.

## 2.2 Fonimu za Kiswahili Sanifu

Kumekuwepo na utata kuhusu idadi kamili ya fonimu za Kiswahili sanifu hii ni kwa sababu wataalam mbalimbali wa isimu katika kazi zao wanatofautiana kuhusu idadi ya fonimu hizi hasa zile za konsonanti. Hata hivyo wote wameziainisha fonimu za Kiswahili sanifu kama:

1. Fonimu za konsonanti
2. Fonimu za irabu
3. Fonimu za nusu irabu

Kulingana na Massamba na wenzake (2004) konsonanti ni aina ya sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondo hewa kutoka mapafuni, ukipitia katika chemba cha kinywa na chemba cha pua kuelekea nje. Ala muhimu zinazohusika na utamkaji wa sauti za aina hii ni ulimi ambao hugusishwa au hufanywa kukaribia sehemu mbalimbali katika chemba cha kinywa. Irabu ni aina ya sauti za lugha ambazo hutamkwa bila kuwepo na kizuizi chochote kwenye mkondo hewa utokao mapafuni ukipitia katika chemba cha kinywa na chemba cha pua. Viyeyusho ni aina ya

vitamkwa ambavyo si konsonanti na wala si irabu yaani huchukuliwa kuwa viko katikati ya irabu na konsonanti. Hii ina maana kwamba kwa kiasi fulani viyeyusho hufanana na konsonanti lakini pia kwa kiasi kikubwa hufanana na irabu katika umbile la utamkaji wake.

### 2.2.1 Fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu

Wataalam mbali mbali wana maoni tofauti tofauti kuhusiana na idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili sanifu. Kwa mfano, Massamba na wenzake (2004) wanaeleza kuwa Kiswahili sanifu kina jumla ya konsonanti 27 zinazotumika katika mfumo wa lugha wa matamshi. Massamba na wenzake wanaeleza kuwa konsonanti za lugha kwa jumla zimekitwa katika misingi mikuu miwili yaani, msingi wa jinsi ya matamshi na msingi wa mahali pa matamshi. Wanaeleza kuwa konsonanti za Kiswahili sanifu pamoja na viyeyusho vyake huainishwa katika makundi saba yafuatayo; vipasuo, vizuio-kwamiza, vikwamizi, nazali, vitambaza, vimadende na viyeyusho ambapo kati ya makundi haya saba, makundi matatu ya mwanzo kutajwa huhusisha konsonanti ambazo zina sifa za ughuna, usoghuna na mpumuo. Wanaeleza kuwa maandishi mengi ya sarufi ya Kiswahili hayajashughulikia sifa ya mpumuo katika konsonanti za Kiswahili kwa kutoa madai kuwa lugha ya Kiswahili sanifu haitofautishi sauti zenye mpumuo na zile ambazo hazina mpumuo ingawa wao katika kazi yao wamezibainisha fonimu zilizo na mpumuo kama vile **/$p^h$/, /$t^h$/, /$k^h$/, /$ts^h$/** kuwa fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu. Iribemwangi (2010) anaeleza kuwa Kiswahili sanifu kina takriban konsonanti 25 na nusu irabu mbili. Katika maelezo yake anaeleza kuwa ametumia neno 'takriban' kimakusudi kwani suala la fonimu za Kiswahili sanifu hukosa ukubaliano miongoni mwa wataalam mbalimbali. Habwe na Karanja (2004) wanabainisha kuwa Kiswahili sanifu kina konsonanti 23 pasipo na kuhusisha viyeyusho. Kihore na wenzake (2001) wanapendekeza kuwa Kiswahili sanifu kina konsonanti 23 na viyeyusho viwili. Mgullu (1999) anadai kuwa Kiswahili kina konsonanti 24. Polome (1967) ameainisha konsonanti ishirini na nne.

Kutokana na maoni tofauti tofauti ya wataalam ambao tumewataja kuhusiana na idadi ya fonimu za Kiswahili sanifu, inaonekana kwamba kuna makubaliano ya kijumla kati yao kuhusu kuwepo kwa fonimu 23 ingawa kuna baadhi ya fonimu za Kiswahili ambazo zinaelekea kuleta mjadala wa kuwepo au kutokuwepo kwake katika Kiswahili sanifu. Mifano ya fonimu hizo ni kama vile **/x/,/ɱ/, /$p^h$/, /$t^h$/, /$k^h$/, /$ts^h$/** . Iribemwangi (2010) pia ameorodhesha fonimu nyingine ambazo pia

huzua utata kuhusu kuwepo kwake katika Kiswahili sanifu. Fonimu hizo ni kama zifuatazo **/mb/, /nd/, /ng/, /nɟ/, /mv/** na /**nz**/. Katika utafiti huu tunachukua mwelekeo wa uainishaji wa Iribemwangi (2010) ambapo tumeziorodhesha konsonanti 23 ambazo hazina utata wowote na pia tumeziorodhesha fonimu ya /ɱ/ na/x/ kwa sababu tumetambua kuwa /ɱ/ hutumika kwa upana sana katika kiswahili sanifu ingawa kuna mwelekeo tofauti unaodai kuwa /**ɱ/** ni alofoni. Vilevile ingawa fonimu /x/ inaonekana kuwa na asili yake katika lugha ya Kiarabu inakubalika kuwa mojawapo ya fonimu ya Kiswahili kwani inatumika kwenye maneno ya Kiswahili. Kulingana na Iribemwangi (2010) konsonanti za Kiswahili sanifu huainishwa katika makundi sita makuu. Makundi hayo ni vipasuo, vizuiwa-kwamizwa, vikwamizwa, nazali, vitambaza na vimadende ingawa Massamba na wenzake (2004) wana mwelekeo tofauti wa uainishaji katika makundi kwani wanaeleza kuwa kwa kuzingatia sifa za jinsi ya matamshi, konsonanti za Kiswahili sanifu pamoja na viyeyusho vyake huainishwa katika makundi saba yafuatayo: vipasuo, vizuio-kwamiza, vikwamizi, nazali, vitambaza, vimadende na viyeyusho.

Vipasuo pia huitwa vizuiwa. Huitwa vipasuo kwa sababu wakati wa kuzitamka hewa huzuiwa katika ala za kutamkia kisha huachiliwa ghafla hivi kwamba sauti hutoka kwa mpasuo. Ubanaji wa hewa hufanywa na midomo kwa baadhi ya vitamkwa na vilevile ulimi katika ufizi na katika kaakaa laini na kunapokuwepo na mrindimo wa nyuzi sauti, vitamkwa vinavyotokea hujulikana kama ghuna na inapokuwa hakuna mrindimo, vitamkwa vinavyopatikana hujulikana kama visoghuna. Kiswahili sanifu kina vipasuo sita ambavyo ni: **/p/, /b/, /t/, /d/, /k/, na /g/** ambapo **/b/, /d/, /g**/ ni ghuna na **/p/, /t/, /k**/ ni visoghuna.

Vizuiwa kwamizwa ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo. Sauti hizi ni mbili katika Kiswahili sanifu ambazo ni **/tʃ/** na /**ɟ/** miongoni mwa vitamkwa hivi /ɟ/ ni ghuna na /tʃ/ ni kisoghuna. Vikwamizwa ni sauti ambazo wakati wa kutamkwa ala za matamshi hukaribiana sana hivi kwamba hewa hupitishwa katikati ya ala hizo hivyo sauti hutokea kwa kukwamizwa. Sauti hizi ni kumi katika Kiswahili sanifu nazo ni **/s/, /z/, /f/, /v/, /Ɵ/, /ð/, /ʃ/, /x/, /ɣ/, /h/**

Nazali ni fonimu ambazo wakati wa kuzitamka hewa nyingi hupitia chemba cha pua na wakati huo kimio kinashuka chini hivi kwamba sauti hizi hutokea kwa king'ong'o. Kiswahili sanifu

kina nazali tano ambazo ni /**m/, /ɱ/, /n/, /ŋ/**, /**ɲ/.** Kuna utata kuhusu fonimu **/ɱ/** kama ni fonimu alofoni ya fonimu /m/. Iribemwangi (2010) anakubali kuwa ni fonimu ambayo hutumika kwa mapana zaidi katika maneno ya Kiswahili sanifu ingawa fonimu hii haijatambuliwa na wataalam wengi hivyo ni muhimu kuiorodhesha kama fonimu ya Kiswahili.

Vitambaza ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka ncha ya ulimi hukita kwenye ufizi na kutatiza mkondo wa hewa huku hewa ikiruhusiwa kupita kando kando mwa ulimi. Kiswahili sanifu kina kitambaza kimoja tu /**l**/.

Wakati wa kutamka sauti za vimadende ncha ya ulimi hupigapiga kwenye ufizi huku hewa ikiendelea kupita na kusababisha mrindimo wa ulimi. Kiswahili sanifu kina kimadende kimoja /r/.

Kiswahili sanifu kina nusu irabu mbili au viyeyusho ambavyo ni /**w/, /j**/. Nusu irabu pia huitwa viyeyusho. /**w/** hutamkwa mdomo ukiwa na mkao wa mviringo na shina la ulimi limevutwa nyuma kuelekea kwenye kaakaa laini. /**j/** hutamkwa midomo ikiwa imetanda huku bapa la ulimi likiwa limeinuliwa kuelekea kaakaa gumu.Wakati wa kutamka sauti hizi, hewa haizuiliwi kama katika kutamka konsonanti na pia hewa haiwachiliwi kama katika irabu.

**Kielelezo 2 Jedwali la konsonanti za Kiswahili sanifu**

| **Mahali pa kutamka** | **Midomo** | **Midomo meno** | **Meno** | **Kaakaa + ufizi** | **Ufizi** | **Kaakaa gumu** | **Kaakaa laini** | **Glota** | **jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo | /p/ /b/ | | | | /t/ /d/ | | /k/ /g/ | | 6 |
| Vizuiwa kwamizwa | | | | | | /tʃ/ /ɟ/ | | | 2 |
| Vikwamizwa | | /f/ /v/ | /ϴ/ /ð/ | /ʃ/ | /s/ /z/ | | /x/ /ɤ/ | /h/ | 10 |
| Nazali | /m/ | /ɱ/ | | | /n/ | /ɲ/ | /ŋ/ | | 5 |
| Kitambaza | | | | | /l/ | | | | 1 |
| Kimadende | | | | | /r/ | | | | 1 |
| Nusu irabu | /w/ | | | | | /j/ | | | 2 |

Asili: Iribemwangi (2010)

### 2.2.2 Fonimu za irabu za Kiswahili Sanifu

Katika Kiswahili sanifu ili kuunda silabi, sauti za konsonanti na irabu huungana hivyo ni muhimu pia kuainisha irabu za Kiswahili sanifu. Kulingana na Iribemwangi (2010) na Mwaliwa (2014), Mgullu (1999) na Massamba na wenzake (2004) lugha nyingi za Kibantu huwa na irabu saba, ilhali Kiswahili sanifu huwa na irabu tano. Kiswahili sanifu kina irabu tano ambazo ni **/i/, /u/, /ɛ/, /ɔ/** na **/a/.** Inadhirika kuwa kuna makubaliano ya kijumla miongoni mwa wataalamkuhusu sifa bainifu za irabu nne zifuatazo /i/, /u/, /ɛ/, /ɔ/ . Hata hivyo suala la sifa ya nyuma ya irabu /a/ inaibua mjadala kwani wataalam mbali mbali wanatoa maelezo tofauti tofauti kuhusiana na fonimu hii kwa mfano Kihore na wenzake (2001) pamoja na Massamba na wenzake (2004) wanaeleza kuwa /a/ ni irabu ya chini-kati iliyo karibu na nyuma. Mgullu (1999) anaeleza kuwa /a/ ni irabu ya chini- kati, Habwe na Karanja (2004) wana msimamo kwamba /a/ ni irabu ya chini-nyuma, Iribemwangi (2010) ana msimamo kwamba /a/ ni irabu ya chini- kati. Utafiti huu una msimamo kwamba /a/ ni irabu ya chini- kati. Sauti za irabu hutamkwa pasipo kuzuiliwa kwa hewa popote kinywani. Vile vile imedhihirika kuwa irabu zote za nyuma huwa na sifa ya [+ mviringo] na irabu za mbele huwa na sifa ya [- mviringo]. Hata hivyo irabu /a/ inaelekea kukiuka madai hayo kwa sababu irabu hii haina sifa ya mviringo kamili au sifa ya tandazwa kamili hivyo hili linachangia kutilia uzito na kuunga mkono madai kuwa /a/ ni irabu ya kati.


Irabu za Kiswahili sanifu huweza kuainishwa kwa kutumia vigezo vitatu ambavyo ni sehemu ya ulimi, hii ni sehemu inayohusika wakati wa kutamka irabu hizi. Inaweza kuwa ya mbele, kati au nyuma. Irabu za mbele katika Kiswahili sanifu ni **/ɛ/,** na **/i/** za nyuma ni **/ɔ/** na **/u/** na irabu ya kati ni **/a/**

Mwinuko wa ulimi unarejelea hali ambapo ulimi unaweza kuinuliwa juu mpaka ukawa sambamba na sehemu ya juu mwa kinywa au unaweza kulazwa chini kinywani au unaweza ukawa katikati mwa kinywa. Irabu zitamkwazo ulimi ukiwa umeinuliwa juu ni za **[**+ juu] ambazo ni **/i/** na **/u/.** Nazo irabu zinazotamkwa ulimi ukiwa katikati ni **/ɛ/** na **/ɔ/.** Irabu ambayo hutamkwa katika sehemu ya chini mwa kinywa ni **/a/.**

Mkao wa mdomo ambapo mdomo unaweza kuwa na mkao wa mviringo au umetandazwa wakati wa kutamka irabu. Irabu zinazotamkwa mdomo ukiwa na mkao wa mviringo ni /ɔ/ na /u/. Irabu zinazotamkwa wakati ambapo mdomo umetandazwa ni **/a/, /ɛ/** na **/i/**. Hata hivyo ni vyema

kufahamu kuwa kiwango cha mviringo au kutanda hutofautiana kulingana na irabu inayohusika. Irabu hizi huweza kuonyeshwa katika mchoro na jedwali lifuatalo.

**Kielelezo 3 Fonimu za irabu za Kiswahili sanifu**




Asili: Iribemwangi (2010)

**Kielelezo 4 Jedwali la irabu za Kiswahili Sanifu**

| Irabu | /i/ | /u/ | /ɛ/ | /ɔ/ | /a/ |
|---|---|---|---|---|---|
| Juu | + | + | - | - | - |
| Chini | - | - | - | - | + |
| Nyuma | - | + | - | + | - |
| Mbele | + | - | + | - | - |
| Mviringo | - | + | - | + | - |
| kaze | + | + | - | - | + |

Asili: Iribemwangi (2010)

Katika kuhitimisha sehemu hii, tulirejelea uainishaji wa fonimu wa Chomsky na Halle (1968) ingawa katika utafiti huu tulitumia mwelekeo wa uainishaji wa fonimu za Kiswahili sanifu wa Iribemwangi (2010). Uainishaji huu ni ule ambao umejikita katika fonetiki matamshi. Kulingana na uainishaji huu ni wazi kuwa kadri irabu inavyokuwa ya juu mbele zaidi ndivyo inavyokuwa ya mbele zaidi na kadri irabu inavyokuwa ya chini- mbele, ndivyo isivyo ya mbele . Hivyo irabu

zote za mbele ni [- mviringo] na zile za nyuma ni [+ mviringo]. Vilevile imebainika wazi kuwa jinsi irabu ya nyuma inavyokuwa juu zaidi ndivyo inavyozidi kuwa ya mviringo zaidi mathalani **/u/** ni ya mviringo zaidi kuliko **/ɔ/** hata ingawa irabu hizo zote ni [+nyuma]. Katika irabu za mbele , jinsi irabu inavyokuwa juu zaidi ndivyo inavyokuwa tandazwa zaidi ndio maana /i/ ni tandazwa zaidi kuliko /ɛ/ ingawa irabu hizi zote ni za mbele.

## 2.3 FONIMU ZA LAHAJA YA KIAMU

Fonimu za lahaja ya Kiamu za konsonanti na irabu zinaelekea kufanana kwa kiwango kikubwa sana na fonimu za Kiswahili sanifu. Tofauti inayojitokeza kati ya fonimu za Kiamu na Kiswahili sanifu ni kwamba fonimu za lahaja hii hasa vipasuo baadhi yake zina sifa ya mpumuo hivyo kuna fonimu za lahaja ya Kiamu zilizo na mpumuo tofauti na inavyodaiwa na wataalam wengi kuwa Kiswahili sanifu hakina fonimu zilizo na mpumuo kwa sababu lugha ya Kiswahili sanifu haitofautishi sauti zenye mpumuo na zile ambazo hazina mpumuo ingawa dhana hii inapingwa na Massamba na wenzake (2004) kwani wanaeleza kuwa Kiswahili sanifu kina fonimu zenye mpumuo na wanaziorodhesha fonimu kama vile **/$p^h$/, /$t^h$/, /$k^h$/, /$ts^h$/** kama fonimu za Kiswahili sanifu kwa sababu katika utafiti walioufanya walibainisha kwamba wasemaji wazawa wa Kiswahili wa pwani ya Afrika Mashariki yote (iwe ni wasemaji wa Kiswahili sanifu au wasemaji wa Kiswahili cha lahaja nyinginezo) umedhihirisha kwamba sifa hii hadi leo imeshamiri sana na hujitokeza waziwazi katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu hata hivyo umekubaliana na madai kuwa Kiswahili sanifu hakina fonimu zenye mpumuo. Utafiti huu umebainisha kuwa konsonanti za lahaja ya Kiamu zimegawika katika makundi sita makuu yafuatayo: vipasuo, vizuiwa-kwamizwa, vikwamizwa, nazali, vitambaza, vimadende . Vile vile kuna viyeyusho viwili katika lahaja ya Kiamu /w/ na /j/.

### Vipasuo

Katika lahaja ya Kiamu sifa ya mpumuo inajitokeza waziwazi hasa katika utamkaji wa baadhi ya vipasuo vyake kama vile /$p^h$/, /$t^h$/, /$k^h$/ na hii ndio tofauti mojawapo inayojitokeza kati ya fonimu za lahaja ya Kiamu na fonimu za Kiswahili sanifu katika utafiti huu. Wakati wa kuzitamka hewa huzuiwa katika ala za kutamkia kisha huachiliwa ghafla ambapo sauti hutoka kwa mpasuo. Katika vipasuo vya lahaja ya Kiamu kuna vile vilivyo ghuna kama vile /b/,/d/, /g/ na vile

visoghuna kama vile /p/, /t/, /k/. Lahaja ya Kiamu ina vipasuo vifuatavyo: **/P/, /$P^h$/, /b/, /t/, /$t^h$/ /d/, /k/, /$k^h$/ na /g/.**

Ifuatayo ni mifano ya maneno tulioipata yenye sauti za vipasuo zenye mpumuo katika utafiti wetu wa lahaja ya Kiamu.

**1.** /$P^h$/ [ $p^h$aa] mnyama wa porini mwembamba na mdogo anayefanana na mbuzi.

/p/ [ paa ] sehemu ya juu ya nyumba.

/$k^h$/ [ $k^h$aa ] mnyama mdogo wa majini

/k/ [ kaa ] kipande cheusi cha kuni kilichochomwa.

/ $t^h$/ **[** $t^h$aa ] aina ya samaki wa majini

/t/ **[** taa **]** kifaa kinachotumiwa kutoa mwanga

Vilevile katika utafiti wetu tulibainisha kwamba fonimu /t/ huweza kutamkwa kwa njia tofauti na wasemaji wa Kiamu kwenye neno moja ili kuibua maana tofauti kati ya neno hilo. Hata hivyo tofauti hii ya kimatamshi huweza kutambuliwa tu na wale wanaoelewa na kuzungumza lahaja hii ya Kiamu hivyo itakuwa vigumu kwa mfano kwa mtu ambaye ni wa bara kuweza kutamka neno hilo na kuibua maana zile tofauti bali atatamka neno hilo kwa njia sawa licha ya kuwa anakusudia kumaanisha vitu tofauti . Neno “mto” linaweza kuibua maana mbili tofauti kutokana na jinsi linavyotamkwa na wasemaji wa lahaja ya Kiamu. Kwa mfano:

**2.** Mto - kitu kama mfuko uliojazwa pamba, sufi au manyoya kinachotumiwa kwa kulazia kichwa wakati wa kulala.

Mto - korongo lenye maji yanayotiririka wakati wote aghalabu kuanzia mlimani kuelekea ziwani au baharini.

Hivyo utaweza tu kubainisha tofauti ya kimaana kutokana na matamshi ya neno hili iwapo unaifahamu lahaja ya Kiamu.

**Vizuiwa Kwamizwa**

Wakati wa kutamka sauti hizi, mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo. Katika lahaja ya Kiamu sauti hizi ni **/tʃ/** na **/ɟ/.** Katika lahaja ya Kiamu tumebaini kuwa wakati mwingine kizuiwa kwamizwa /tʃ/ hutamkwa kama /t/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu kutokana na athari ya lahaja ya Kiamu katika Kiswahili kwa mfano:

**3.** kuchukua hutamkwa kama kutukua

machozi hutamkwa kama matozi.

Pia tulitambua kuwa kizuiwa-kwamizwa /ɟ/ huweza kutamkwa kama /j/ katika baadhi ya maneno ya lahaja ya Kiamu. Kwa mfano:

**4.** pamoja hutamkwa kama pamoya

moja hutamkwa kama moya

**Vikwamizwa**

Sauti hizi zinapotamkwa ala za matamshi hukaribiana sana hivi kwamba hewa hupitishwa katikati ya ala hizo hivyo sauti hutokea kwa kukwamizwa. Sauti hizi ni: **/s/, /z/, /f/, /v/, /Ɵ/, /ð/, /ʃ/, /x/, /ɤ/, /h/.**

Tulitambua kuwa katika baadhi ya maneno ya lahaja ya Kiamu, kikwamizwa **/v/** hutamkwa kama /z/. Kwa mfano:

**5.** vitu hutamkwa kama zitu

vijana hutamkwa kama zijana

vyombo hutamkwa kama zombo

Pia tulitambua kuwa maneno mengi yaliyo na kikwamizwa /x/ huwa ni maneno yenye asili ya Kiarabu ingawa yanakubalika kutumika katika lahaja ya Kiamu.

**Nazali**

Katika kuzitamka sauti hizi, hewa nyingi hupitia chemba cha pua hivi kwamba sauti hizi hutokea kwa king'ong'o. Lahaja ya Kiamu ina nazali zifuatazo**/m/, /ɱ/, /n/, /ŋ/, /ɲ/**

**Vitambaza**

Wakati wa kuzitamka sauti hizi ncha ya ulimi hukita kwenye ufizi na kutatiza mkondo wa hewa na hewa hupitia kando kando mwa ulimi. Lahaja ya Kiamu ina kitambaza kimoja **/l/.** Tulibaini kuwa wakati mwingine katika baadhi ya maneno ya lahaja ya Kiamu kitambaza /l/ kinapojitokeza katikati ya irabu mbili huishia kudondoshwa kwa mfano,

**6.** mbee badala ya mbele

Kae badala ya kale

**Vimadende**

Sauti hizi zinapotamkwa ncha ya ulimi hupigapiga kwenye ufizi huku hewa ikipita na kusababisha mrindimo wa ulimi. Lahaja ya Kiamu ina kimadende kimoja **/r**/. Tulitambua kuwa wakati mwingine fonimu /r/ inapojitokeza katikati ya irabu mbili katika maneno ya lahaja ya Kiamu huishia kudondoshwa wakati wa kutamka kwa mfano,

**7.** chua badala ya kutamkwa kama chura.

### 2.3.1 Viyeyusho/ nusu irabu

Wakati wa kutamka sauti hizi, hewa haizuiliwi kama katika kutamka konsonanti na pia hewa haiwachiliwi kama katika irabu. Lahaja ya Kiamu ina nusu irabu zifuatazo **/w/, /j/**

**Kielelezo 5 Jedwali la konsonanti za lahaja ya Kiamu**

| **Mahali pa kutamka** | **Midomo** | **Midomo meno** | **Meno** | **Kaakaa + ufizi** | **Ufizi** | **Kaakaa gumu** | **Kaakaa laini** | **Glota** | **jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo | /p/ /b/ /P$^h$/ | | | | /t/ /d/ t$^h$ | | /k/ /g/ k$^h$ | | 9 |
| Vizuiwa kwamizwa | | | | | | /tʃ/ /ɟ/ | | | 2 |
| Vikwamizwa | | /f/ /v/ | /Ɵ/ /ð/ | /ʃ/ | /s/ /z/ | | /x/ /ɣ/ | /h/ | 10 |
| Nazali | /m/ | /ɱ/ | | | /n/ | /ɲ/ | /ŋ/ | | 5 |
| Kitambaza | | | | | /l/ | | | | 1 |
| Kimadende | | | | | /r/ | | | | 1 |
| Nusu irabu | /w/ | | | | | /j/ | | | 2 |


Asili: Utafiti wetu tulioufanya

### 2.3.2 Fonimu za irabu za lahaja ya Kiamu

Ili kuunda silabi katika maneno ya lahaja ya Kiamu tuligundua kwamba, sauti za konsonanti na irabu huungana kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili sanifu. Lahaja ya Kiamu huwa na irabu tano ambazo ni **/a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/** na **/u/**. Irabu hizi huweza kuainishwa kwa kutumia vigezo vitatu ambavyo ni sehemu ya ulimi, mwinuko wa ulimi na mkao wa mdomo kama tulivyoelezea awali

katika uainishaji wa irabu za Kiswahili Sanifu.  Irabu za lahaja ya Kiamu zinaweza kuwasilishwa katika mchoro kama ifuatavyo:

**Kielelezo 6    Fonimu za irabu za lahaja ya Kiamu**




Asili: Utafiti wetu tuliofanya

Hivyo irabu zote za mbele ni [- mviringo] na zile za nyuma ni [+ mviringo]. Vilevile imebainika wazi kuwa jinsi irabu ya nyuma inavyokuwa juu zaidi ndivyo inavyozidi kuwa ya mviringo zaidi mathalani /u/ ni ya mviringo zaidi kuliko /ɔ/ hata ingawa irabu hizo zote ni [+nyuma]. Katika irabu za mbele, jinsi irabu inavyokuwa juu zaidi ndivyo inavyokuwa tandazwa zaidi ndio maana /i/ ni tandazwa zaidi kuliko /ɛ/ ingawa irabu hizi zote ni za mbele.

**Kielelezo 7   Matriki ya irabu za lahaja ya Kiamu**

| Irabu | /i/ | /u/ | /ɛ/ | /ɔ/ | /a/ |
|---|---|---|---|---|---|
| Juu | + | + | - | - | - |
| Chini | - | - | - | - | + |
| Nyuma | - | + | - | + | - |
| Mbele | + | - | + | - | - |
| Mviringo | - | + | - | + | - |
| Kaze | + | + | - | - | + |

Asili: Utafiti wetu

## 2.4 FONIMU ZA LAHAJA YA KITIKUU

Katika uchunguzi wetu tulibainisha kuwa lahaja ya Kitikuu ina fonimu zifuatazo: konsonanti, irabu na viyeyusho. Konsonanti za lahaja ya Kitikuu ziko katika makundi sita makuu. Makundi hayo ni vipasuo, vizuiwa kwamizwa, vikwamizwa, nazali, vitambaza na vimadende. Tulitambua kuwa fonimu za konsonanti za lahaja ya Kitikuu zinaelekea kuwa sawa na konsonanti za Kiswahili sanifu kwani tofauti iliopo ni kidogo sana hasa katika Kitikuu ambapo tunachukua mwelekeo kuwa hakuna kikwamizwa /z/. Pia katika lahaja hii kuna fonimu zilizo na mpumuo tofauti na ilivyo katika Kiswahili sanifu ingawa kuna wataalam wanaopinga dhana hii. Tulitambua kuwa fonimu /z/ inapojitokeza katika maneno hutamkwa kama /ð/ katika takriban maneno yote hata katika majina ya watu. Kwa mfano,

**8.** Zote hutamkwa kama dhote.
Maziwa hutamkwa kama madhiwa.

**Vipasuo**

Sauti hizi huitwa vipasuo kwa sababu wakati wa kuzitamka hewa huzuiliwa katika ala za kutamkia na kisha huachiliwa ghafla ambapo sauti hizi hutoka kwa nguvu au mpasuo. Lahaja ya Kitikuu ina vipasuo vifuatavyo: **/p/, /$p^h$/, /b/, /t/,/ $t^h$/, /d/, /k/, /$k^h$/** na **/g/.** Katika utafiti huu tulitambua kuwa wakati mwingine kipasuo /t/ katika maneno huishia kutamkwa kama /tʃ/. Kwa mfano maneno yafuatayo:

**9.** Tatu hutamkwa kama chachu
Mti hutamkwa kama mchi

Hata hivyo tulitambua kuwa sio wakati wote ambapo /t/ hutamkwa kama /tʃ/ kwa mfano maneno kama vile:

**10.** tena hutamkwa kama tena.
tayari hutamkwa kama tayari.

**Vizuiwa Kwamizwa**

Wakati wa kuzitamka sauti hizi, hewa huzuiliwa kwenye kaakaa gumu kisha huachiliwa ghafla lakini mkondo hewa haufunguliwi wote na kwa sababu hiyo hewa hutoka kwa kutatizika na hivyo kusababisha mkwamzo. Lahaja ya Kitikuu ina vizuiwa kwamizwa vifuatavyo **/tʃ/** na **/ɟ/.**

Tulitambua kuwa wakati mwingine kizuiwa kwamizwa /ɟ/ katika maneno ya Kiswahili hutamkwa kama /j/ kwa mfano maneno yafuatayo:

**11.** Maji hutamkwa kama mayi

Moja hutamkwa kama moya.

Hata hivyo hili halijitokezi katika maneno yote yaliyo na kizuiwa-kwamizwa /ɟ/ kwani kuna maneno mengine ambayo hayabadiliki kama vile,

**12.** jeuri, japo, ajabu hutamkwa kama yalivyo.

Vile vile wakati mwingine katika maneno, kizuiwa-kwamizwa /ɟ/ hutamkwa kama kipasuo /d/. Kwa mfano maneno yafuatayo:

**13.** njaa hutamkwa kama ndaa

nje hutamkwa kama nde

**Vikwamizwa**

Katika kutamka sauti hizi, ala za matamshi kama vile meno na ulimi hukaribiana sana na kuifanya hewa kupitishwa katikati ya ala hizi kwa kukwamizwa hivyo sauti hizi hutokea kwa kukwamizwa. Sauti hizi ni tisa katika lahaja ya Kitikuu. Nazo ni: **/s/, /f/, /v/, /Ɵ/, /ð/, /ʃ/, /h/, /ɤ/** na **/x/.** Katika utafiti huu tulitambua kuwa kikwamizwa /v/ wakati mwingine katika maneno hutamkwa kama /ð/ kwa mfano,

**14.** viatu hutamkwa kama dhiachu.

viazi hutamkwa kama dhiadhi.

**Nazali**

Katika kutamka sauti hizi, hewa hufungiwa katika bomba la sauti kisha huachiliwa kupitia kwenye chemba cha pua na vile vile wakati huo kimio hushuka chini na kusababisha mkondo hewa wa pua kuzitoa sauti hizo kwa king'ong'o. Lahaja ya Kitikuu ina nazali zifuatazo **/m/, /ɱ/, /n/, /ŋ/** na **/ɲ/.** Tulitambua kuwa wakati mwingine maneno yanapotangulizwa na nazali /m/ na kufuatiwa na baadhi ya vipasuo kama vile /k/ na /t/, nazali /m/ hugeuka na kutamkwa kama /n/ kwa mfano:

**15.** nkache badala ya mkate.

nchu badala ya mtu.

**Kitambaza**

Katika kutamka sauti hii, ncha ya ulimi hukita kwenye ufizi na kutatiza mkondo hewa hivyo hewa hulazimika kupitia kando kando mwa ulimi. Lahaja ya Kitikuu huwa na kitambaza kimoja tu **/l/.** Tulitambua pia kuwa kitambaza /l/ hudondoshwa kinapojitokeza kati kati ya irabu mbili kwa mfano:

**16.** kuea badala ya kulea.

**Kimadende**

Hutamkwa wakati ambapo ncha ya ulimi hugotagota kwenye ufizi na hewa hupita na kusababisha mrindimo wa ulimi. Lahaja ya Kitikuu huwa na kimadende kimoja ambacho ni **/r/.**

### 2.4.1 Viyeyusho/ nusu irabu

Lahaja ya Kitikuu ina viyeyusho viwili ambavyo ni **/w/** na **/j/.** Tulitambua kuwa katika baadhi ya maneno, kiyeyusho **/w/** hugeuka na kutamkwa kama **/v**/ kwa mfano:

**17.** wageni hutamkwa kama vageni.
wasichana hutamkwa kama vasichana.

**Kielelezo 8 Jedwali la konsonanti za lahaja ya Kitikuu**


| **Mahali pa kutamka** | **Midomo** | **Midomo meno** | **Meno** | **Kaakaa + ufizi** | **Ufizi** | **Kaakaa gumu** | **Kaakaa laini** | **Glota** | **jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo | /p/ /b/ /pʰ/ | | | | /t/ /d/ /tʰ/ | | /k/ /g/ /kʰ/ | | 9 |
| Vizuiwa kwamizwa | | | | | | /tʃ/ /ɟ/ | | | 2 |
| Vikwamizwa | | /f/ /v/ | /Ɵ/ /ð/ | /ʃ/ | /s/ | | /x/ /ɤ/ | /h/ | 9 |
| Nazali | /m/ | /ɱ/ | | | /n/ | /ɲ/ | /ŋ/ | | 5 |
| Kitambaza | | | | | /l/ | | | | 1 |
| Kimadende | | | | | /r/ | | | | 1 |
| Nusu irabu | /w/ | | | | | /j/ | | | 2 |

Asili: Utafiti wetu

### 2.4.2 Fonimu za irabu za lahaja ya Kitikuu

Lahaja ya Kitikuu huwa na irabu tano ambazo ni **/a/, /e/, /i/, /ɔ/,** na **/u/.** Sauti hizi za irabu hutamkwa pasipo kuzuiliwa kwa hewa popote kinywani. Irabu hizi huainishwa kwa kutumia vigezo vitatu ambavyo ni: Sehemu ya ulimi, mwinuko wa ulimi na mkao wa mdomo kama tulivyoelezea katika fonimu za Kiswahili sanifu. Irabu za lahaja ya Kitikuu zinaweza kuwasilishwa katika mchoro kama ifuatavyo:

**Kielelezo 9 Fonimu za irabu za lahaja ya Kitikuu**




Asili: Utafiti wetu

Hivyo irabu zote za mbele ni [- mviringo] na zile za nyuma ni [+ mviringo]. Vilevile imebainika wazi kuwa jinsi irabu ya nyuma inavyokuwa juu zaidi ndivyo inavyozidi kuwa ya mviringo zaidi mathalani **/u/** ni ya mviringo zaidi kuliko **/ɔ/** hata ingawa irabu hizo zote ni [+nyuma]. Katika irabu za mbele, jinsi irabu inavyokuwa juu zaidi ndivyo inavyokuwa tandazwa zaidi ndio maana /i/ ni tandazwa zaidi kuliko /ε/ ingawa irabu hizi zote ni za mbele.

**Kielelezo 10 Matriki ya irabu za lahaja ya Kitikuu**

| Irabu | /i/ | /u/ | /ɛ/ | /ɔ/ | /a/ |
|---|---|---|---|---|---|
| Juu | + | + | - | - | - |
| Chini | - | - | - | - | + |
| Nyuma | - | + | - | + | - |
| Mbele | + | - | + | - | - |
| Mviringo | - | + | - | + | - |
| kaze | + | + | - | - | + |

Asili: Utafiti wetu.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia fonimu za Kiswahili sanifu na fonimu za lahaja za Kiamu na Kitikuu. Aidha, tumetoa sifa bainifu za fonimu za Konsonanti na za irabu za lahaja hizi tatu.Vilevile tumeziwasilisha fonimu za konsonanti na irabu za lahaja hizi zote katika jedwali. Kutokana na utafiti huu tumetambua kuwa fonimu za lugha ya Kiswahili sanifu zinaelekea kuwa na mfanano mkubwa na fonimu za lahaja za Kiamu na Kitikuu kwa sababu tulitambua kuwa sauti za irabu katika lahaja hizi tatu ni sawa na vilevile tuligundua kwamba nyingi ya konsonanti za lahaja hizi zilikuwa zinafanana ingawa kuna chache zilizokuwa tofauti . Hata hivyo tulitambua kwamba kuna tofauti katika fonimu za kila mojawapo ya lahaja hizi kwa mfano tulitambua kwamba lugha ya Kiswahili sanifu haina sauti zenye mpumuo ilhali lahaja za Kiamu na Kitikuu zina sauti zenye mpumuo kama tulivyozijadili. Tulitambua pia kwamba kila mojawapo ya lahaja hizi zilikuwa na viyeyusho viwili ambavyo ni /w/ na /j/. Kwa ujumla tulibainisha kwamba lahaja ya Kiamu ilikuwa na konsonanti 28 na viyeyusho viwili ilhali lahaja ya Kitikuu ilikuwa na konsonanti 27 na viyeyusho viwili. Mwelekeo tulioutumia katika utafiti huu ni kuwa Kiswahili sanifu kina konsonanti 25 na viyeyusho viwili.

# SURA YA TATU

# ATHARI ZA KISAUTI KATIKA KISWAHILI SANIFU KUTOKANA NA LAHAJA YA KIAMU

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia athari zinazodhihirika kimaandishi na kimatamshi miongoni mwa wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kiamu kama lugha yao ya kwanza wanapotumia Kiswahili sanifu. Aidha katika sura hii tumeonyesha mifano ya baadhi ya maneno inayoonyesha kuwepo kwa athari hizo ambapo tumeyaandika maneno hayo kama yanavyotamkwa na kuandikwa katika lahaja ya Kiamu na pia katika Kiswahili sanifu. Athari hizi hutokana na ule uzoefu wa wazungumzaji hawa kutumia lahaja hii ya Kiamu katika miktadha mingi maishani mwao hivyo inakuwa vigumu kwao kujiepusha na uhamishaji wa baadhi ya sifa za lahaja ya Kiamu na kuziingiza katika muktadha ambapo wazungumzaji hawa wanatumia Kiswahili sanifu. Maneno hayo wanayotamka au kuandika hudhihirisha kukiukwa kwa mfumo wa sauti za Kiswahili sanifu unaokubalika au unaozoeleka katika matumizi yake. Hii ni kwa sababu kama ilivyo katika lugha zingine kila lugha huwa na miundo ya maneno inayofaa kufuatwa kama vile sauti zipi zinazoweza kufuatana na zipi katika mazingira fulani, Kiswahili sanifu kina mfumo wa sauti mahususi ambao unafaa kufuatwa ili kukitumia kwa usahihi na iwapo kanuni hizo katika Kiswahili sanifu zitakiukwa na wanafunzi hawa katika kazi zao huishia kubainika kuwa ni makosa.

Athari hizi za kisauti huibua utata wa kimaana ambapo wakati mwingine maana huweza kupotea kabisa au kuvurugwa. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa matatizo ya athari za kisauti yalijitokeza zaidi katika sauti za konsonanti ambapo wanafunzi tuliowachunguza ambao lahaja ya Kiamu ndio lugha yao ya kwanza waligeuza baadhi ya konsonanti za Kiswahili sanifu kwa kuzitumia kama wanavyozitumia konsonanti hizi katika lahaja ya Kiamu kutokana na hali ya kuwa na uzoefu wa kuzungumza lahaja hii. Tulitambua pia kuwa baadhi ya wanafunzi tuliochunguza insha zao walidondosha sauti ya konsonanti iwapo imejitokeza katikati ya irabu mbili kama vile tutakavyoonyesha katika mifano ya maneno kama yalivyoandikwa na wanafunzi katika insha zao.

Aidha katika sura hii tumeeleza sababu ambazo huenda zilisababisha kutokea kwa kila mojawapo ya athari ya kisauti tuliyoijadili kwa kuzingatia michakato mitano ya nadharia ya Lugha Kati tuliyoijadili hapo awali kama mihimili mikuu katika utafiti wetu. Vilevile katika uchanganuzi wa data katika sura hii tumetumia mchoro wa mviringo wa asilimia ili kuonyesha ni asilimia ngapi ya wanafunzi tuliowachunguza ambao walidhihirisha kuwa na athari fulani au kutokuwa na athari hiyo katika matumizi yao ya Kiswahili sanifu. Pia tumetoa maelezo ya kufafanua kila kielelezo cha mchoro wa asilimia ili kuweza kubainisha iwapo athari fulani ilionekana kuenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza au ilidhihirika tu miongoni mwa wanafunzi wachache tuliowachunguza. Athari za kisauti zinazotokana na data yetu ni kama zifuatazo:

### 3.2.1 Matumizi ya /j/ badala ya /ɟ /

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kiamu kama lugha yao ya kwanza wanapojifundisha Kiswahili sanifu hutamka sauti /ɉ/ kama /ɟ/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu na hili ndilo huchangia kupatikana kwa miundo isiyokubalika katika Kiswahili sanifu hivyo kubainika kama makosa katika lugha ya Kiswahili sanifu. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha athari hii katika kazi andishi tulizozichunguza.


| | **Kiamu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| **18.** | moya | [mɔja] | moja | [mɔɟa] |
| | yua | [jua] | jua | [ɟua] |
| | pamoya | [pamɔja] | pamoja | [pamɔɟa] |
| | mayani | [majani] | majani | [maɟani] |

Fonimu /j/ na /ɟ/ ni sauti ambazo hutamkwa kwenye kaakaa gumu hata hivyo kuna tofauti kati ya sauti hizi kwani /ɟ/ ni kizuiwa kwamizwa hivyo wakati wa kutamka sauti hii, mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo ilhali sauti /j/ ni nusu irabu ambapo ni sauti ambayo wakati wa kutamka hakuna mkwamzo au kutatiziwa sana kwa mkondo hewa. Hivyo tulitambua kuwa wanafunzi hawa huishia kuhamisha sifa hii wanapoyatamka maneno ya

Kiswahili sanifu na hili huwasababishia kuibuka na athari hii katika maandishi na matamshi yao katika lugha ya Kiswahili sanifu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati sababu ambayo huenda ilichangia kutokea kwa athari hii ni kutokana na mchakato wa mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili kama tulivyojadili katika nadharia ya Lugha Kati kuwa katika juhudi za kuwalisilisha maana katika mawasiliano ya lugha lengwa mwanafunzi hutumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano ili aweze kuwasilisha maana hivyo tuligundua kuwa wanafunzi tuliowachunguza walitumia /j/ katika baadhi ya maneno katika insha zao kutokana na uzoefu wao wa kutumia sauti hii katika lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kiamu.

**Kielelezo 11   Mchoro wa matumizi ya   /j/ badala ya /ɟ /**




Kutokana na kielelezo 11 hapo juu imedhihirika kuwa miongoni mwa wanafunzi ambao tulichunguza insha zao, athari hii ya matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/ ilijitokeza kwa kiwango kikubwa mno cha asilimia themanini na tatu. Hata hivyo tunaona kuwa kuna idadi ndogo ya asilimia kumi na saba ya wanafunzi ambao hawakuwa na athari hii katika kazi walizoziandika. Kutokana na kielelezo hiki ni wazi kwamba athari hii ilikuwa imeenea sana miongoni mwa wanafunzi.


### 3.2.2 Matumizi ya /z/ badala ya /v/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu yaliyo na sauti ya kikwamizwa /v/ ikitangulia katika neno, sauti hii hutamkwa kama /z/ na baadhi ya wanafunzi tuliowachunguza ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kiamu. Sauti hizi mbili zina sifa mbalimbali zinazofanana kama vile (+ konsonanti, + kikwamizwa, + ghuna) hata hivyo kuna tofauti kati yazo ambayo ni kuwa /v/ hutamkiwa katika midomo- meno ilhali /z/ hutamkiwa kwenye ufizi.

Kulingana na nadharia ya Lugha Kati sababu ambayo huweza kusababisha kuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi ni kutokana na mchakato wa uhamishaji lugha asilia ambapo wanafunzi hawa ambao wamezoea kuzungumza lahaja ya Kiamu kama lugha yao ya kwanza ambapo sauti /v/ mara nyingi hutamkwa kama /z/ hivyo wanafunzi hawa huishia kuhamisha sifa hii ya kutamka /v/ kama /z/ kutokana na mazoea waliyo nayo katika lugha yao asilia ya Kiamu. Sababu nyingine huenda ikawa ni kutokana na mchakato wa uhamishaji wa yaliyosomwa ambapo wanafunzi hawa hutamka na kuandika maneno haya kama walivyojifundisha kutoka kwa walimu wao au vitabu wanavyovisoma hivyo iwapo vitabu hivyo au walimu hawa watakuwa na athari hii katika matamshi au maandishi yao basi athari hii itaishia kurithishwa kwa wanafunzi hawa wanaojifundisha Kiswahili sanifu. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha athari hii ya matumizi ya /z/ badala ya /v/. Pia tuliweza kuonyesha kiwango cha kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza kwa kutumia mchoro wa asilimia uliopo hapo chini.

| | **Kiamu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| **19.** | ziazi. | [ziazi] | viazi | [viazi] |
| | zijana | [ziɟana] | vijana | [viɟana] |
| | ziatu | [ziatu] | viatu | [viatu] |
| | zitu | [zitu] | vitu | [vitu] |

**Kielelezo 12 Mchoro wa matumizi ya /z/ badala ya /v/**




Kutokana na kielelezo 12 imedhihirika wazi kwamba miongoni mwa wanafunzi ambao tulichunguza insha zao takriban asilimia sitini na tano ya wanafunzi hawakuwa na athari hii ya kutamka au kuandika sauti /v/ kama /z/ katika insha zao. Hata hivyo tulipata wanafunzi wachache takriban asilimia thelathini na tano ya wanafunzi hao walikuwa na athari hii katika uandishi wa insha zao tulizozichunguza. Kutokana na kielelezo hiki tulibainisha kwamba athari hii haikuwa imeenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

### 3.2.3 Matumizi ya /d/ badala ya /z/


Miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kiamu kama lugha yao ya kwanza tulitambua kuwa wanapoyatamka au kuyaandika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu hubadilisha sauti /z/ na kutamka kama /d/ hasa inapotanguliwa na nazali /n/. Sauti hizi hutamkwa katika ufizi, ni konsonanti na ni sauti ghuna. Hata hivyo sauti hizi zina tofauti kwani /d/ ni kipasuo ilhali /z/ ni kikwamizwa. Mifano ya maneno iliyodhihirisha athari hii katika data yetu ni kama vile:

| | Kiamu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **20.** | kwanda | [kwanda] | kwanza | [kwanza] |

| | | | |
|---|---|---|---|
| fundwa | [fundwa] | funzwa | [funzwa] |
| nilianda | [nilianda] | nilianza | [nilianza] |
| kuanda | [kuanda] | kuanza | [kuanza] |

Kulingana na nadharia ya Lugha Kati sababu ambayo huenda ilisababisha kuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ni kutokana na mchakato wa uhamishaji lugha asilia ambapo wanafunzi wanahamisha mazoea au sifa za lugha yao ya kwanza na kuziingiza katika maneno ya Kiswahili sanifu. Sababu nyingine ambayo huweza kuchangia kuwepo kwa athari hii ni uhamishaji wa yaliyosomwa ambapo wanafunzi huishia kutumia kanuni wanazojifundisha kutoka kwa walimu, wazazi au vitabu. Hivyo iwapo walimu au wazazi wana athari hii ya kubadili sauti /z/ wakati wanafundisha au kuzungumza lugha ya Kiswahili sanifu basi athari hii huishia kurithishwa kwa wanafunzi hawa kama tulivyoshuhudia miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

**Kielelezo 13 Mchoro wa matumizi ya /d/ badala ya /z/**




Kutokana na kielelezo 13 imedhihirika kuwa takriban asilimia hamsini ya wanafunzi tuliochunguza insha zao walikuwa na athari hii ya kutumia /d/ badala ya /z/ katika insha zao. Pia imedhihirika kuwa takriban asilimia hamsini ya wanafunzi tuliochunguza insha zao hawakuwa na athari hii katika insha zao hivyo imedhihirika kuwa athari hii ilikuwa imeenea kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi.

### 3.2.4 Matumizi ya /t/ badala ya /tʃ/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kiamu kama lugha yao ya kwanza wanapojifundisha Kiswahili sanifu walidhihirisha athari hii katika insha zao ambapo wanaandika na kutamka sauti /tʃ/ kama /t/. /tʃ/ ni kizuiwa- kwamizwa hivyo wakati wa kuitamka, mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo. /t/ ni kipasuo ambapo wakati wa kutamka sauti hii hewa huzuiwa katika ala za kutamkia kisha huachiliwa ghafla ambapo sauti hutoka kwa mpasuo. Mifano ya athari hii kutokana na data yetu ni kama vile:


| | **Kiamu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| **21.** | kitwa | [kitwa] | kichwa | [kitʃwa] |
| | matozi | [matɔzi] | machozi | [matʃɔzi] |
| | nilitukua | [nilitukua] | nilichukua | [nilitʃukua] |
| | tini | [tini] | chini | [tʃini] |

Kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati athari hii huenda hujitokeza miongoni mwa wanafunzi wanaojifundisha Kiswahili sanifu kutokana na sababu kama vile uhamishaji wa lugha asilia ambapo wanafunzi hawa walihamisha na kuunda vitambulisho vya lugha kwa kupanua vipengele vya kiisimu vya lahaja ya Kiamu na kuvichukulia kuwa vina maana sawa katika Kiswahili sanifu na hili ndilo husababisha kuibuka kwa lugha kati miongoni mwa wanafunzi hawa kwani lugha wanayojifundisha na kuzungumza au kuiandika ni lugha iliyo kati ya lahaja ya Kiamu na Kiswahili sanifu. Sababu nyingine ambayo huenda ilisababisha kuwepo kwa athari hii ni uhamishaji wa yaliyosomwa ambapo wanafunzi hawa hurithi athari hizi kutoka kwa walimu, wazazi au vitabu na hili huweza kusababisha kutokea kwa makosa katika Kiswahili sanifu kama ilivyobainika katika insha za wanafunzi tulizozichunguza katika utafiti wetu.

Mchakato wa mbinu za mawasiliano vilevile huenda ukawa mojawapo ya sababu zinazochangia kutokea kwa athari hii kwani ni mbinu inayotumiwa na wanafunzi kusuluhisha matatizo ya kimawasiliano hasa wakati mwanafunzi anapohisi kuwa kipengele cha kiisimu kinachohitajika hakipatikani hili humfanya mwanafunzi kuibua miundo na ruwaza mbalimbali za kiisimu ili

aweze kuwasilisha maana katika mawasiliano yake na ruwaza hizi huishia kuwa za kudumu katika lugha kati hii ya wanafunzi na hili hudhihirika kama makosa kama tulivyotambua katika kazi za wanafunzi za Kiswahili sanifu tulizozitafitia kwani tulitambua kuwa wanafunzi wengine walitumia maneno na sauti za lugha yao ya kwanza (Kiamu) katika juhudi za kuwasilisha maana katika insha za Kiswahili sanifu walizoziandika.

**Kielelezo 14 Mchoro wa matumizi ya /t/ badala ya /tʃ/**




Kutokana na kielelezo 14 imebainika kuwa asilimia sabini ya wanafunzi tuliochunguza insha zao hawakuwa na athari hii ya kutamka au kuandika sauti /tʃ/ kama /t/. Vilevile tumebainisha kuwa takriban asilimia thelathini ya wanafunzi tuliochunguza insha zao walikuwa na athari hii katika kazi walizoziandika hivyo tuligundua kwamba athari hii haikuenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

### 3.2.5 Matumizi ya /d/ badala ya /ɟ/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwepo kwa athari hii miongoni mwa kazi andishi za Kiswahili sanifu za wanafunzi tuliowachunguza ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kiamu ambapo sauti /ɟ/ ilitamkwa na kuandikwa kama /d/ hasa inapotanguliwa na nazali /n/ katika neno.


| | Kiamu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **22.** | ndoo | **[**ndɔɔ] | njoo | [ɲɟɔɔ] |

| | | | |
|---|---|---|---|
| uwanda | [uwanda] | uwanja | [uwaɲɟa] |
| ndaa | [ndaa] | njaa | [ɲɟaa] |
| ndia | [ndia] | njia | [ɲɟia] |

Mojawapo ya sababu kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati ambazo huenda zilichangia kuibuka kwa athari hii katika kazi hizo za wanafunzi tulizozichunguza ni kutokana na uhamishaji wa lugha asilia ambapo wanafunzi hawa wanahamisha maana ya vitu na matamshi ya maneno kutoka katika mfumo wa lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kiamu na kuingiza maana hiyo katika Kiswahili sanifu. Uhamishaji wa yaliyosomwa pia huenda ukawa ni sababu iliyochangia kutokea kwa athari hii. Hii ni kwa sababu wanafunzi hawa wanaojifundisha lugha ya Kiswahili sanifu hutumia kanuni walizojifundisha kutoka kwa walimu au vitabu hivyo iwapo walimu hawa wanaowafundisha wana athari hii wataishia kuirithisha athari hii kwa wanafunzi jambo ambalo tulishuhudia katika insha za wanafunzi tulizozichunguza.

Mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili pia huenda ikawa ni mojawapo ya sababu ya kutokea kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi . Hili hutokea wakati ambapo mwanafunzi anataka kusuluhisha matatizo ya kimawasiliano na kuwasilisha maana hivyo mwanafunzi huyu hulazimika kutumia baadhi ya vipengele vya kiisimu vya lugha yake asilia ili kuweza kuwasilisha maana aliyokusudia kama tulivyotambua katika insha za wanafunzi ambapo tulipata maneno au sauti za lahaja ya Kiamu zimetumiwa na wanafunzi katika insha zao kwa lengo la kuwasilisha maana katika uandishi wao.

**Kielelezo 15 Mchoro wa athari katika matumizi ya /d/ badala ya /ɟ /**




Kulingana na kielelezo 15 imedhihirika kuwa takriban asilimia sitini na saba ya wanafunzi ambao tulichunguza insha zao hawakuwa na athari hii. Pia mchoro huu umebainisha kuwa takriban asilimia thelathini na tatu ya wanafunzi tuliochunguza insha zao walikuwa na athari hii ya kutamka /d/ badala ya /ɟ/ katika insha zao. Hivyo kutokana na mchoro huu tuliweza kutoa msimamo kwamba idadi kubwa ya wanafunzi tuliowachunguza hawakukumbwa na athari hii katika Kiswahili sanifu kutokana na lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kiamu.

### 3.2.6 Udondoshaji wa /l/ katika maneno


Katika uchunguzi wetu wa kazi andishi za wanafunzi tulizozichunguza tuligundua kuwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kiamu wanapoyatamka au kuandika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu hudondosha sauti /l/. Tuligundua kuwa sauti hii hudondoshwa inapotokea katikati ya irabu mbili katika neno. Mifano ya athari hii katika data yetu ni kama ifuatavyo:

| | Kiamu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **23.** | kueta | [kuɛta] | kuleta | [kulɛta] |
| | kae | [kaɛ] | kale | [kalɛ] |
| | mbee | [mbɛɛ] | mbele | [mbɛlɛ] |
| | kuea | [kuɛa] | kulea | [kulɛa] |

Kulingana na nadharia ya Lugha Kati sababu mojawapo ambayo huenda ilisababisha kuwepo kwa athari hii miongoni mwa kazi za wanafunzi tulizozichunguza ni kutokana na mchakato wa ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa ambapo mwanafunzi huonyesha ithibati ya kuwa ameshika kanuni ya kijumla lakini hajui ni lini kanuni hiyo haitumiki na pia makosa haya ya ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa huonyesha ni mambo yepi mengine ambayo mwanafunzi hajapata kujifundisha. Katika Kiswahili sanifu kuna kanuni ya udondoshaji ambapo katika baadhi ya maneno sauti za irabu au konsonanti hudondoshwa ingawa kuna mipaka au sheria ambayo huzingatiwa katika kanuni hii kama vile huwa tunasema “walimu” badala ya “waalimu”.

Katika insha tulizozichunguza tulitambua kuwa kanuni hii ya udondoshaji wa sauti katika Kiswahili sanifu ilikiukwa na baadhi ya wanafunzi kwani walihamisha baadhi ya sifa za udondoshaji wa sauti katika lugha asilia yao ambapo kulingana na insha tulizozichunguza tulitambua kuwa katika lahaja ya Kiamu mara nyingi konsonanti hudondoshwa katika baadhi ya maneno inapotokea katikati ya irabu mbili na hivyo wanafunzi wanapohamisha sifa hii ya kudondosha konsonanti katika maneno iwapo inatokea katikati ya irabu mbili katika kuandika insha za Kiswahili sanifu inadhihirika kuwa ni makosa.

**Kielelezo 16 Mchoro wa athari ya udondoshaji wa /l/ katika maneno**



Kutokana na kielelezo 16 imebainika wazi kwamba takriban asilimia ishirini na tano ya wanafunzi tuliowachunguza walikuwa na athari ya kudondosha sauti /l/ katika baadhi ya maneno katika insha walizoziandika. Imebainika pia kwamba takriban asilimia sabini na tano ya wanafunzi tuliowachunguza katika insha zao hawakuwa na athari hii katika kazi zao. Kutokana na kielelezo hiki tulitambua kwamba athari hii haikuwa imeenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

## 3.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeonyesha baadhi ya athari za kisauti za lahaja ya Kiamu katika Kiswahili sanifu tulizozitambua katika kazi andishi za wanafunzi tuliowachunguza. Kutokana na uchunguzi huo tuligundua kuwa wanafunzi wengi tuliowachunguza walikuwa na athari ya kutumia sauti /j/ badala ya /ɟ/ katika Kiswahili sanifu. Aidha tulitambua kuwa kuwepo na kutokuwepo kwa athari ya matumizi ya /d/ badala ya /z/ kulikuwa kwa asilimia hamsini hivyo tulitambua kuwa nusu ya wanafunzi tuliowachunguza walikuwa na athari hii katika insha walizoziandika ilhali nusu nyingine ya wanafunzi tuliowachunguza hawakudhihirisha athari hii katika insha zao. Tulitambua pia kwamba athari ya udondoshaji wa /l/ katika maneno ya Kiswahili sanifu haikudhihirika kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza kwani takriban asilimia sabini na tano ya wanafunzi hawakuwa na athari hii.
Aidha tumeeleza visababishi vya kutokea kwa athari hizo katika kazi za wanafunzi tuliowachunguza.

Miongoni mwa sababu tulizozitambua kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati ni kama vile uhamishaji lugha asilia ambapo wanafunzi huhamisha baadhi ya sifa kutoka lugha ya kwanza na kuziingiza katika lugha ya pili wanayojifundisha. Uhamishaji wa yaliyosomwa, mbinu za mawasiliano katika lugha lengwa na ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa pia ni sababu nyingine tulizozitambua kwamba husababisha kutokea kwa athari hizo. Vilevile tumetumia kielelezo cha mchoro wa mviringo wa asilimia ili kuonyesha viwango vya athari hizo katika insha za Kiswahili sanifu za wanafunzi tuliowachunguza ambapo athari ya matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/ ilijitokeza kwa kiwango kikubwa na athari ya udondoshaji wa sauti /l/ katika maneno ya Kiswahili sanifu ilijitokeza kwa kiwango cha chini zaidi miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

# SURA YA NNE

# ATHARI ZA KISAUTI KATIKA KISWAHILI SANIFU KUTOKANA NA LAHAJA YA KITIKUU

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia athari zinazodhihirika kimaandishi miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja ya Kitikuu wanapotumia Kiswahili sanifu. Tumeonyesha mifano ya baadhi ya maneno tuliyoyapata katika kazi andishi za wanafunzi kutoka shule mbalimbali zilizo katika kisiwa cha Lamu yanayoonyesha kuwepo kwa athari za kisauti pamoja na jinsi maneno hayo yanavyonuiwa kuandikwa na kutamkwa katika Kiswahili sanifu na wazungumzaji hao. Kila lugha huwa na miundo ya maneno inayotakiwa kufuatwa ili kuitumia kwa usahihi kwa mfano ni sauti zipi zinazofaa kufuatana na zipi na katika mazingira yepi. Hivyo iwapo mtumizi wa lugha ya Kiswahili atazihamisha au kubadilisha sauti za lugha, ataishia kuivuruga miundo ya maneno na sauti za lugha ya Kiswahili sanifu na hili ndilo husababisha kutokea kwa makosa kama tulivyobainisha katika insha za wanafunzi tulizozichunguza.

Athari hizi za kisauti aghalabu huishia kuvuruga maana na hivyo huibua utata wa kimaana ambapo maana hupotea kabisa au huweza kubadilika. Katika lahaja ya Kitikuu tulitambua kuwa athari hizi za kisauti hujitokeza zaidi katika sauti za konsonanti ambapo wanafunzi hutumia konsonanti za Kitikuu wanapoandika maneno ya Kiswahili sanifu. Aidha katika sura hii tumeeleza ni sababu zipi ambazo huenda zilichangia kutokea kwa athari hizo za kisauti miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza kwa kurejelea michakato mitano ya nadharia ya Lugha Kati tuliyoijadili hapo awali. Pia tumetumia kielelezo cha mchoro wa asilimia katika kila mojawapo ya athari tuliyoijadili ili kuonyesha ni asilimia ngapi ya wanafunzi tuliowachunguza waliodhihirisha kuwa na au kutokuwa na athari hizo. Kutokana na michoro hiyo tuliweza kubainisha ni athari zipi zilizokuwa zimeenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza na vilevile tuliweza kutambua ni athari zipi hazikuwa zimeenea kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza. Athari za kisauti tulizozipata kutokana na data yetu ni kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Matumizi ya /tʃ/ badala ya /t/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kitikuu kama lugha yao ya kwanza wanapojifundisha Kiswahili sanifu hutamka sauti /t/ kama

/tʃ/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu na hili huchangia kutokea kwa miundo ya maneno isiyokubalika katika Kiswahili sanifu hivyo huonekana kuwa ni makosa. Fonimu /t/ ni sauti ya konsonanti iliyo katika kikundi cha kizuiwa kwamizwa na hutamkiwa kwenye kaakaa gumu. Fonimu hizi mbili zina sifa moja inayofanana kwamba sauti hizi mbili hazina mghuno. Hivyo kutokana na maelezo yetu hapo awali tulitambua kuwa sauti hizi zina tofauti nyingi kuliko kuwepo na mfanano kati yazo kwani wakati wa kutamka /t/ hewa huzuiwa katika ala za kutamkia kisha huachiliwa ghafla hivi kwamba sauti hii hutoka kwa mpasuo ilhali wakati wa kutamka /tʃ/ mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo. Ifuatayo ni mifano ya maneno inayodhihirisha athari hii katika kazi andishi za wanafunzi tuliowachunguza.


| | **Kitikuu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| **24.** | chachu | [tʃatʃu] | tatu | [tatu] |
| | nchu | [ntʃu] | mtu | [mtu] |
| | vachu | [vatʃu] | watu | [watu] |
| | kwechu | [kwɛtʃu] | kwetu | [kwɛtu] |

Kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati sababu mojawapo ambayo huenda ilichangia kuibuka kwa athari hii ni kutokana na mchakato wa uhamishaji wa lugha asilia ambapo wanafunzi huhamisha sifa hii ya kutamka sauti /t/ kama /tʃ/ kutokana na uzoefu walionao katika lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kitikuu na wanafunzi hawa wanapohamisha sifa hii katika Kiswahili sanifu inaishia kuibuka kama makosa kwani inasababisha kuibuka kwa miundo ya maneno isiyokubalika katika Kiswahili sanifu.

Mchakato wa mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili au lengwa huenda ukawa pia ni sababu iliyochangia kutokea kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambapo katika juhudi za kuwasilisha maana katika mawasiliano, mwanafunzi hulazimika kutumia baadhi ya vipengele vya lugha ya kwanza hasa wakati kipengele anachokihitaji hakipatikani au hakitambui kama njia ya kufidia upungufu huo na kuibua maana aliyokusudia katika lugha anayojifundisha. Hivyo wanafunzi tuliowachunguza katika insha zao walidhihirisha athari hii kutokana na uzoefu wao wa kutumia sauti hiyo katika lugha yao ya kwanza ingawa madhumuni yao huwa ni

kuwasilisha maana katika insha zao. Tuliwasilisha matokeo yetu ya uchunguzi wetu kuhusu athari hii katika mchoro uliopo hapo chini.

**Kielelezo 17 Mchoro wa matumizi ya /tʃ/ badala ya /t/**




Kutokana na kielelezo 17 hapa juu imedhihirika kwamba miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza asilimia hamsini ya wanafunzi hao walidhihirisha kuwa na athari hii katika insha zao ikilinganishwa na asilimia hamsini ya wanafunzi ambao hatukupata athari hii katika insha walizoziandika hivyo athari hii ilikuwa katika hali ya wastani kwani nusu ya wanafunzi tuliowachunguza walidhihirisha kutokuwa na athari hii. Hata hivyo ilionekana kuwa imeenea sana miongoni mwa wanafunzi.

### 4.2.2 Matumizi ya /ð/ badala ya /z/

Katika uchunguzi wetu tuligundua kwamba sauti /z/ hutamkwa kama /ð/ na wanafunzi tuliowachunguza ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kitikuu na ambao wanajifundisha Kiswahili sanifu kama lugha ya pili au zaidi. Sauti hizi mbili zina mfanano mkubwa kwani zote ni sauti za konsonanti, pia ni vikwamizwa na vilevile ni sauti zilizo na mghuno. Hata hivyo kuna tofauti moja kuhusu mahala pa kutamkia kwani sauti /z/ hutamkwa kwenye ufizi ilhali sauti /ð/ hutamkwa kwenye meno. Wakati wa kutamka sauti hizi ala za kutamkia hukaribiana sana hivi kwamba hewa hupitishwa katikati ya ala hizo hivyo sauti hutokea kwa kukwamizwa. Katika utafiti wetu tulichukulia kwamba lahaja ya Kitikuu haina fonimu /z/ ndiposa baadhi ya wanafunzi tuliowachunguza walikuwa wakitumia /ð/ badala ya /z/ katika kuandika maneno


katika insha za Kiswahili sanifu. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha kuwepo kwa athari hii katika kazi andishi za wanafunzi tuliowachunguza.

| | Kitikuu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **25.** | kadhi | [kaði] | kazi | [kazi] |
| | ndhuri | [nðuri] | nzuri | [nzuri] |
| | mwedhi | [mwɛði] | mwezi | [mwɛzi] |
| | matodhi | [matɔði] | machozi | [matʃɔzi] |

Sababu mojawapo kulingana na nadharia ya Lugha Kati ambayo huenda ilisababisha kutokea kwa athari hii ni kutokana na mchakato wa uhamishaji wa yaliyosomwa ambapo wanafunzi tuliowachunguza hutamka maneno katika Kiswahili sanifu kama wanavyojifundisha kutoka kwa walimu wao au kutokana na vitabu wanavyovisoma hivyo iwapo walimu hawa watakuwa na athari hii katika matamshi au maandishi ya Kiswahili sanifu basi athari hii itarithishwa kwa wanafunzi hawa wanaojifundisha Kiswahili sanifu na huenda miundo ya maneno wanayoibuka nayo huishia kuwa ya kudumu hivyo wataendelea kuitumia katika matamshi au maandishi yao kama tulivyoshuhudia katika baadhi ya insha za wanafunzi tulizozichunguza.

Mchakato wa uhamishaji wa lugha asilia pia huenda ukawa ni sababu nyingine iliyochangia kutokea kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambapo wanafunzi hawa huwa wamezoea kuzungumza lahaja ya Kitikuu kama lugha yao ya kwanza ambapo sauti /z/ hutamkwa kama /ð/ hivyo wanafunzi hawa huishia kuhamisha sifa hii hadi katika Kiswahili sanifu kutokana na mazoea waliyo nayo katika lugha ya kwanza. Tuliweza kuwasilisha matokeo ya asilimia ya kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza katika mchoro ufuatao.

**Kielelezo 18   Mchoro wa matumizi ya /ð/ badala ya /z/**




Kutokana na kielelezo 18 hapo juu imebainika kwamba asilimia hamsini ya wanafunzi tuliowachunguza walidhihirisha kuwa walikuwa na athari hii ya kutamka sauti /z/ kama /ð/. Imebainika pia kwamba asilimia hamsini ya wanafunzi tuliowachunguza hawakuwa na athari hii katika insha walizoziandika hivyo athari hii inaonekana kuwa imeenea kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi wanapotumia Kiswahili sanifu.


### 4.2.3   Matumizi ya /v/ badala ya /w/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu sauti /w/ hutamkwa kama /v/ na baadhi ya wanafunzi tuliowachunguza ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kitikuu. Sauti hizi mbili zinafanana katika baadhi ya sifa kama vile sauti hizi ni ghuna na ni konsonanti. Hata hivyo sauti hizi zina tofauti kwani /v/ ni kikwamizwa hivyo wakati wa kutamka sauti hii ala za matamshi hukaribiana sana na hewa hupitishwa katikati ya ala hizo hivyo sauti hutokea kwa kukwamizwa na sauti hii hutamkiwa kwenye midomo meno. /w/ ni sauti inayotamkiwa kwenye mdomo na ni nusu irabu. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha kuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

| | Kitikuu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **26.** | vageni | [vagɛni] | wageni | [wagɛni] |
| | vengi | [vɛŋgi] | wengi | [wɛŋgi] |
| | vachu | [vatʃu] | watu | [watu] |
| | vengine | [vɛŋginɛ] | wengine | [wɛŋginɛ] |

Kwa kurejelea nadharia ya Lugha Kati athari hii huenda ilijitokeza miongoni mwa wanafunzi wanaojifundisha Kiswahili sanifu kutokana na sababu kama vile uhamishaji wa lugha asilia ambapo wanafunzi hawa walihamisha na kuunda vitambulisho vya lugha kwa kupanua vipengele vya kiisimu vya lahaja ya Kitikuu na kuvichukulia kuwa vina maana sawa katika Kiswahili sanifu na hili ndilo husababisha kuibuka kwa makosa au athari hizi. Sababu nyingine ambayo huweza kuchangia kuwepo kwa athari hii ni uhamishaji wa yaliyosomwa ambapo wanafunzi hutumia kanuni wanazojifundisha kutoka kwa walimu, wazazi au vitabu. Hivyo iwapo walimu au wazazi hao wana athari hii ya kubadili sauti /w/ wakati wanafundisha lugha ya Kiswahili sanifu basi athari hii huishia kurithishwa kwa wanafunzi kama tulivyotambua katika insha za wanafunzi tuliowachunguza. Tuliweza kuwasilisha kiwango cha kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii katika mchoro ufuatao.

**Kielelezo 19  Mchoro wa matumizi ya /v/ badala ya /w/**




Kielelezo 19 kinadhihirisha kwamba miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza katika uandishi wao wa insha asilimia hamsini na tatu yao walikuwa na athari hii ya kutamka sauti /w/ kama /v/. Pia imebainika wazi kwamba asilimia arobaini na saba ya wanafunzi tuliowachunguza hawakudhihirisha athari hii katika insha zao. Kutokana na kielelezo hiki ni bayana kuwa athari hii imeenea kwa kiasi kikubwa miongoni mwa wanafunzi.


### 4.2.4 Matumizi ya /ð/ badala ya /vy/ au /v/

Miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kitikuu kama lugha yao ya kwanza tulitambua kuwa wanapoyatamka au kuyaandika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu hutamka sauti /vy/ au /v/ kama /ð/. Sauti /v/ na /ð/ huwa na mfanano mkubwa kwani zote ni konsonanti, ni vikwamizwa na vilevile ni sauti zenye mghuno. Tofauti iliopo baina ya sauti hizi ni kwamba /v/ hutamkiwa kwenye midomo-meno ilhali /ð/ hutamkiwa kwenye meno. Ifuatayo ni mifano ya maneno inayodhihirisha kuwepo kwa athari hii katika insha tulizozichunguza.

| | Kitikuu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **27.** | dhombo | [ðɔmbɔ] | vyombo | [vjɔmbɔ] |
| | dhote | [ðɔtɛ] | vyote | [vjɔtɛ] |
| | dhechu | [ðɛtʃu] | vyetu | [vjɛtu] |
| | dhao | [ðaɔ] | vyao | [vjaɔ] |

Kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati mchakato wa mbinu za mawasiliano huenda ukawa mojawapo ya sababu zinazochangia kutokea kwa athari hii kwani ni mbinu inayotumiwa na wanafunzi wanaojifundisha lugha ili kusuluhisha matatizo ya kimawasiliano hasa wakati mwanafunzi anapohisi kuwa kipengele cha kiisimu kinachohitajika hakipatikani hili humfanya mwanafunzi kuibua miundo na ruwaza mbalimbali za kiisimu ili aweze kuwasillisha maana katika mawasiliano yake ambapo ruwaza hizi huwa za kudumu katika lugha kati hii ya mwanafunzi ingawa hudhihirika kama makosa katika Kiswahili sanifu kama tulivyoshuhudia katika insha za wanafunzi tulizozichunguza. Uhamishaji wa lugha asilia pia huenda ikawa sababu ya kutokea kwa athari hii ambapo wanafunzi huhamisha maana ya vitu au matamshi ya maneno kutoka kwa lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kitikuu na kuingiza matamshi hayo na maana hizo katika Kiswahili sanifu. Tuliweza kuwasilisha matokeo yetu kuhusu kiwango cha kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza katika mchoro ufuatao:

**Kielelezo 20  Mchoro wa matumizi ya /ð/ badala ya /v/ au /vy/**




Kwa mujibu wa kielelezo 20 imedhihirika kwamba asilimia hamsini ya wanafunzi tuliowachunguza walikuwa na athari hii ya kutamka sauti /v/ au /vy/ kama /ð/ katika insha zao ilhali asilimia hamsini ya wanafunzi tuliowachunguza hawakudhihirisha athari hii katika insha zao. Tuliweza kubainisha kuwa athari hii ilikuwa imeenea kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi hivyo walimu wanapaswa kutafuta mbinu ya kusuluhisha tatizo hili.


### 4.2.5 Matumizi ya /n/ badala ya /m/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu, wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kitikuu kama lugha ya kwanza hutamka sauti /m/ kama /n/ hasa iwapo neno hilo limeanza kwa nazali /m/ na ikifuatana na sauti kama vile /t/, /k/, /l/, /s/, /ʃ/, na /d/. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha kuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

| | Kitikuu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **28.** | nkache | [nkatʃɛ] | mkate | [mkatɛ] |
| | nchu | [ntʃu] | mtu | [mtu] |
| | nke | [nkɛ] | mke | [mkɛ] |
| | nshahara | [nʃahara] | mshahara | [mʃahara] |

Kulingana na nadharia ya Lugha Kati sababu mojawapo ambayo huenda ilisababisha kuwepo kwa athari hii miongoni mwa kazi za wanafunzi tulizozichunguza ni kutokana na mchakato wa ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa ambapo mwanafunzi huonyesha ithibati ya kuwa ameshika kanuni ya kijumla lakini hajui ni lini kanuni hiyo hutumika au kutotumika. Mchakato wa uhamishaji lugha asilia pia huenda ukawa sababu ya kutokea kwa athari hii ambapo wanafunzi wanahamisha mazoea au sifa za lugha yao ya kwanza kama vile tulivyoshuhudia katika baadhi ya insha za wanafunzi tulizozichunguza ambapo walikuwa wakibadilisha sauti /m/ na kuiandika kama /n/ kutokana na jinsi walivyozoea kubadilisha sauti hii katika lugha yao ya kwanza. Tuliweza kuwasilisha katika mchoro ufuatao asilimia ya kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

**Kielelezo 21 Mchoro wa matumizi ya /n/ badala ya /m/**



Kutokana na kielelezo 21 imebainika kwamba wanafunzi wengi tuliowachunguza walikuwa na athari hii katika insha zao ambapo asilimia sabini ya wanafunzi hao walidhihirisha athari hii katika insha zao ikilinganishwa na asilimia thelathini ya wanafunzi ambao hatukupata athari hii katika insha zao. Kutokana na haya ni wazi kwamba athari hii ilikuwa imeenea sana miongoni mwa wanafunzi.

### 4.2.6 Matumizi ya /t/ badala ya tʃ/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kitikuu kama lugha yao ya kwanza wanapojifundisha Kiswahili sanifu walidhihirisha athari hii katika insha zao ambapo wanaandika na kutamka sauti /tʃ/ kama /t/. /tʃ/ ni kizuiwa kwamizwa hivyo wakati wa kuitamka sauti hii mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo. /t/ ni kipasuo ambapo wakati wa kutamka sauti hii hewa huzuiwa katika ala za kutamkia kisha huachiliwa ghafla ambapo sauti hutoka kwa mpasuo. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha kuwepo kwa athari hii katika insha za wanafunzi tuliowachunguza.


| | **Kitikuu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| **29.** | mtana | [mtana] | mchana | [mtʃana] |
| | kutukua | [kutukua] | kuchukua | [kutʃukua] |
| | huata | [huata] | huacha | [huatʃa] |
| | mtwa | [mtwa] | mchwa | [mtʃwa] |

Mchakato wa mbinu za mawasiliano kulingana na nadharia ya Lugha Kati huenda ukawa mojawapo ya sababu zinazochangia kutokea kwa athari hii kwani ni mbinu inayotumiwa na wanafunzi kusuluhisha matatizo ya kimawasiliano hasa wakati mwanafunzi anapohisi kuwa kipengele cha kiisimu kinachohitajika hakipatikani hili humfanya mwanafunzi kuibua miundo na ruwaza mbalimbali za kiisimu ili aweze kuwasilisha maana katika mawasiliano yake na ruwaza hizi huishia kuwa za kudumu katika lugha kati hii ya wanafunzi na hili hudhihirika kama makosa

kama tulivyotambua katika kazi za wanafunzi za Kiswahili sanifu tulizozitafitia kwani tulitambua kuwa wanafunzi wengine walitumia maneno na sauti za lugha yao ya kwanza (Kitikuu) katika juhudi za kuwasilisha maana katika insha za Kiswahili sanifu walizoziandika.

Athari hii pia huenda ilijitokeza miongoni mwa wanafunzi wanaojifundisha Kiswahili sanifu kutokana na sababu kama vile uhamishaji wa lugha asilia ambapo wanafunzi hawa walihamisha na kuunda vitambulisho vya lugha kwa kupanua vipengele vya kiisimu vya lahaja ya Kitikuu na kuvichukulia kuwa vina maana sawa katika Kiswahili sanifu na hili ndilo husababisha kuibuka kwa lugha kati miongoni mwa wanafunzi hawa kwani lugha wanayojifundisha na kuzungumza au kuiandika ni lugha iliyo kati ya lahaja ya Kitikuu na Kiswahili sanifu. Sababu nyingine ambayo huenda ilisababisha kuwepo kwa athari hii ni uhamishaji wa yaliyosomwa ambapo wanafunzi hawa hurithi athari hizi kutoka kwa walimu, wazazi au vitabu na hili huweza kusababisha kutokea kwa makosa katika Kiswahili sanifu kama ilivyobainika katika insha za wanafunzi tulizozichunguza katika utafiti wetu. Tulitumia mchoro ufuatao kuonyesha asilimia ya wanafunzi tuliowachunguza ambao walidhihirisha athari hii na wasiokuwa na athari hii katika insha zao.

**Kielelezo 22  Mchoro wa matumizi ya /t/ badala ya /tʃ/**



Kutokana na kielelezo 22 inabainika kwamba miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza wengi wao hawakuwa na athari hii katika insha zao kwani ni asilimia thelathini tu ya wanafunzi hawa waliodhihirisha athari hii katika insha walizoziandika. Asillimia sabini ya wanafunzi tuliowachunguza hawakudhihirisha athari hii katika insha zao hivyo ni wazi kwamba athari hii haijaenea sana miongoni mwa wanafunzi.

### 4.2.7 Matumizi ya /d/ badala ya /ɟ /

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwepo kwa athari hii miongoni mwa kazi andishi za Kiswahili sanifu za wanafunzi tuliowachunguza ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kitikuu ambapo sauti /ɟ/ hutamkwa kama /d/ katika baadhi ya maneno iwapo inatanguliwa na nazali /n/ katika neno. Tuliorodhesha mifano ifuatayo ilyoonyesha kuwepo kwa athari hii katika insha za wanafunzi tuliowachunguza.


| | Kitikuu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **30.** | ndaa | [ndaa] | njaa | [ɲɟaa] |
| | nde | [ndɛ] | nje | [ɲɟɛ] |
| | ndiani | [ndiani] | njiani | [ɲɟiani] |
| | uwandani | [uwandani] | uwanjani | [uwaɲɟani] |

Kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati mojawapo ya sababu ambazo huenda zilichangia kuibuka kwa athari hii katika kazi hizo za wanafunzi tulizozichunguza ni kutokana na uhamishaji wa lugha asilia ambapo wanafunzi hawa wanahamisha maana ya vitu na matamshi ya maneno kutoka katika mfumo wa lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kitikuu na kuingiza maana hiyo katika Kiswahili sanifu. Uhamishaji wa yaliyosomwa pia huenda ukawa ni sababu iliyochangia kutokea kwa athari hii. Hii ni kwa sababu wanafunzi hawa wanaojifundisha lugha ya Kiswahili sanifu hutumia kanuni walizojifundisha kutoka kwa walimu au vitabu hivyo iwapo walimu hawa wanaowafundisha wana athari hii wataishia kuirithisha athari hii kwa wanafunzi jambo ambalo tulishuhudia katika insha za wanafunzi tulizozichunguza.

Mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili pia huenda ikawa ni mojawapo ya sababu ya kutokea kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi . Hili hutokea wakati ambapo mwanafunzi anataka

kusuluhisha matatizo ya kimawasiliano na kuwasilisha maana hivyo mwanafunzi huyu hulazimika kutumia baadhi ya vipengele vya kiisimu vya lugha yake asilia ili kuweza kuwasilisha maana aliyokusudia kama tulivyotambua katika insha za wanafunzi ambapo tulipata maneno au sauti za lahaja ya Kitikuu zimetumiwa na wanafunzi katika insha zao kwa lengo la kuwasilisha maana katika uandishi wao. Tulitumia mchoro ufuatao kuonyesha kiwango cha kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

**Kielelezo 23  Mchoro wa matumizi ya /d/ badala ya /ɟ/**




Kielelezo 23 kinadhihirisha kwamba miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza wengi wao hawakuwa na athari hii ya kutamka /ɟ/ kama /d/ katika insha walizoziandika kwani inabainika kwamba ni asilimia thelathini tu ya wanafunzi tuliowachunguza ambao walikuwa na athari hii katika insha walizoziandika hivyo asilimia sabini ya wanafunzi tuliowachunguza hawakuwa na athari hii katika insha zao hivyo ni wazi kwamba athari hii haijaenea kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi.

### 4.2.8 Matumizi ya /n/ badala ya /ɲ/


Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu, wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kitikuu hutamka sauti /ɲ/ kama /n/ kama ilivyodhihirika katika baadhi ya insha za wanafunzi tulizozichunguza. Sauti hizi mbili zina

mfanano mkubwa kwani zote ni nazali, ni sauti ghuna na ni konsonanti. Tofauti iliyopo kati yazo ni kuwa /n/ hutamkiwa kwenye ufizi ilhali /ɲ/ hutamkiwa kwenye kaakaa gumu. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha kuwepo kwa athari hii katika insha za wanafunzi tuliowachunguza.

| | Kitikuu | | Kiswahili sanifu | |
|---|---|---|---|---|
| **31.** | numbani | [numbani] | nyumbani | [ɲumbani] |
| | noka | [nɔka] | nyoka | [ɲɔka] |
| | kunwa | [kunwa] | kunywa | [kuɲwa] |
| | kinwaji | [kinwaɟi] | kinywaji | [kiɲwaɟi] |

Sababu ambayo huenda ilichangia kutokea kwa athari hii kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati ni kutokana na mchakato wa mbinu za mawasiliano katika lugha lengwa na uhamishaji wa lugha asilia ambapo katika juhudi za kuwasilisha maana katika mawasiliano ya lugha lengwa mwanafunzi hutumia mikakati mbalimbali ili aweze kuwasilisha maana ambapo mojawapo ya mikakati hiyo ni kuhamisha sifa ya kutamka sauti /ɲ/ kama /n/ kutokana na uzoefu wao katika lugha yao ya kwanza. Hivyo wanafunzi hawa wanapoandika /n/ badala ya /ɲ/ katika maneno ya Kiswahili sanifu inaishia kuibuka kama makosa. Tulitumia mchoro ufuatao kuonyesha asilimia ya kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

**Kielelezo 24   Mchoro wa matumizi ya /n/ badala ya /ɲ/**




Kutokana na kielelezo 24 imedhihirika kwamba asilimia ishirini na nane ya wanafunzi tuliowachunguza walikuwa na athari hii ya kutumia /ɲ/ badala ya /n/ katika insha zao ilhali tulibainisha kwamba asilimia sabini na mbili ya wanafunzi tuliowachunguza hawakudhihirisha athari hii katika insha zao hivyo tulitambua kuwa athari hii haikuenea sana miongoni mwa wanafunzi katika sehemu tuliofanya utafiti wetu.

### 4.2.9   Matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/

Katika uchunguzi wetu tulitambua kuwa wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kitikuu kama lugha yao ya kwanza wanapojifundisha Kiswahili sanifu hutamka sauti /ɟ/ kama /j/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu na hili ndilo huchangia kupatikana kwa miundo isiyokubalika katika Kiswahili sanifu hivyo kubainika kama makosa katika lugha ya Kiswahili sanifu. Ifuatayo ni mifano ya maneno iliyodhihirisha athari hii katika kazi andishi tulizozichunguza.


| | **Kitikuu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| **32.** | | | | |
| | miyi | [miji] | miji | [miɟi] |

| | | | |
|---|---|---|---|
| mayi | [maji] | maji | [maɟi] |
| umeyaa | [umɛjaa] | umejaa | [umɛɟaa] |
| mmoya | [mmɔja] | mmoja | [mmɔɟa] |

Fonimu /ɟ/ na /j/ ni sauti ambazo hutamkwa kwenye kaakaa gumu hata hivyo kuna tofauti kati ya sauti hizi kwani /ɟ/ ni kizuiwa kwamizwa hivyo wakati wa kutamka sauti hii, mkondo hewa huzuiwa kisha kuachiliwa taratibu na kutoka kwa mkwamzo ilhali sauti /j/ ni nusu irabu ambapo ni sauti ambayo wakati wa kutamka hakuna mkwamzo au kutatiziwa sana kwa mkondo hewa. Hivyo tulitambua kuwa wanafunzi hawa huishia kuhamisha sifa hii wanapoyatamka maneno ya Kiswahili sanifu na hili huwasababishia kuibuka na athari hii katika maandishi na matamshi yao katika lugha ya Kiswahili sanifu.

Kulingana na nadharia ya Lugha Kati sababu ambayo huenda ilichangia kutokea kwa athari hii ni kutokana na mchakato wa mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili kama tulivyojadili katika nadharia ya Lugha Kati kuwa katika juhudi za kuwalisilisha maana katika mawasiliano ya lugha lengwa mwanafunzi hutumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano ili aweze kuwasilisha maana hivyo tuligundua kuwa wanafunzi tuliowachunguza walitumia /j/ katika baadhi ya maneno katika insha zao kutokana na uzoefu wao wa kutumia sauti hii katika lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kitikuu. Tulitumia mchoro ufuatao kuonyesha asilimia ya kuwepo na kutokuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza

**Kielelezo 25 Matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/**




Kielelezo 25 kinadhihirisha kwamba athari hii ya matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/ ilidhihirika kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza kwani asilimia themanini na tatu ya wanafunzi tuliowachunguza walidhihirisha kuwa na athari hii katika insha zao huku asilimia kumi na saba pekee ya wanafunzi tuliowachunguza ndio hawakuwa na athari hii katika insha walizoziandika. Kutokana na haya ni bayana kwamba athari hii imeenea kwa kiwango kikubwa mno miongoni mwa wanafunzi katika sehemu tuliofanyia utafiti wetu.

### 4.2.10 Udondoshaji wa /m/, /l/, na /j/ katika maneno


Katika uchunguzi wetu wa insha za wanafunzi tuliowachunguza tuligundua kuwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kitikuu wanapotamka au kuandika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu hudondosha baadhi ya sauti kama tutakavyoonyesha katika mifano. Tuligundua kuwa sauti /l/ hudondoshwa inapotokea katikati ya irabu mbili katika neno la lahaja ya Kitikuu na kuhamisha sifa hii katika maneno ya Kiswahili sanifu. Vilevile tulitambua kwamba fonimu /m/ hudondoshwa inapotokea kabla ya irabu /i/ ambapo katika uchunguzi wetu tulibainisha kwamba athari hii ilijitokeza tu katika neno “mimi” katika insha za wanafunzi tuliowachunguza. Pia tulitambua kwamba fonimu /j/ ilidondoshwa katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu katika insha za wanafunzi tuliowachunguza ambapo sauti hii hudondoshwa hasa katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu ambayo ni vivumishi vimilikishi na vya pekee

kama tutakavyoonyesha katika mifano. Ifuatayo ni mifano ya maneno inayoonyesha athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

| | **Kitikuu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|---|
| **33.** | imi | [imi] | mimi | [mimi] |
| | angu | [aŋgu] | yangu | [jaŋgu] |
| | echu | [ɛtʃu] | yetu | [jɛtu] |
| | kueta | [kuɛta] | kuleta | [kulɛta] |

Kulingana na nadharia ya Lugha Kati athari hii huenda ilisababishwa na mchakato wa ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa ambapo mwanafunzi huonyesha ithibati ya kwamba ameshika kanuni ya kijumla lakini hajui ni lini kanuni hiyo haitumiki. Kwa mfano katika Kiswahili sanifu kuna kanuni ya udondoshaji ambapo katika baadhi ya maneno sauti za irabu na konsonanti hudondoshwa ingawa kuna mipaka yake. Katika insha tulizozichunguza tulitambua kuwa baadhi ya wanafunzi walikiuka kanuni za udondoshaji katika Kiswahili sanifu kwa sababu walihamisha sifa ya kudondosha sauti hizo kama walivyozoea katika lahaja ya Kitikuu na hili husababisha kutokea kwa makosa katika Kiswahili sanifu kwa sababu maneno yanayoundwa hayakubaliki katika Kiswahili sanifu kwani yana muundo tofauti hivyo hubainishwa kama makosa. Tuliweza kuwasilisha kuwepo kwa athari hii miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza katika mchoro ufuatao.

**Kielelezo 26   Mchoro wa athari ya udondoshaji wa /m/, /l/ na /j/**




Kutokana na kielelezo 26 imedhihirika kwamba asilimia arobaini na tatu ya wanafunzi tuliowachunguza walikuwa na athari hii ya kudondosha sauti hizi katika insha walizoziandika ilhali asilimia hamsini na saba ya wanafunzi tuliowachunguza hawakudhihirisha kuwa na athari hii katika insha walizoziandika hivyo tulibainisha kwamba athari hii haikuwa imeenea sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza.

## 4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeonyesha baadhi ya athari za kifonolojia za lahaja ya Kitikuu katika Kiswahili sanifu tulizozitambua katika kazi andishi za wanafunzi tuliowachunguza. Kutokana na uchunguzi huo tuligundua kuwa wanafunzi wengi tuliowachunguza walikuwa na athari ya kutumia sauti /j/ badala ya /ɟ/ katika Kiswahili sanifu. Athari ya matumizi ya /n/ badala ya /m/ pia ilionekana kuwepo kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi wengi tuliowachunguza kwani asilimia sabini ya wanafunzi tuliowachunguza walidhihirisha kuwa na athari hii katika insha zao. Pia tulitambua kuwa kuwepo na kutokuwepo kwa athari ya matumizi ya /ð/ badala ya /v/ au/vy/ kulikuwa kwa asilimia hamsini hivyo tulitambua kuwa nusu ya wanafunzi tuliowachunguza walikuwa na athari hii katika insha walizoziandika ilhali nusu nyingine ya wanafunzi tuliowachunguza hawakudhihirisha athari hii katika insha zao. Tulitambua pia kwamba athari ya matumizi ya /n/ badala ya /ɲ/ katika maneno ya Kiswahili sanifu

haikudhihirika kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza kwani takriban asilimia sabini na mbili ya wanafunzi tuliochunguza insha zao hawakuwa na athari hii.

Aidha tumeeleza sababu mbalimbali kwa mujibu wa nadharia ya Lugha Kati ambazo huweza kuchangia kutokea kwa athari hizo katika kazi za wanafunzi tuliowachunguza. Miongoni mwa sababu tulizozitambua ni kama vile uhamishaji lugha asilia ambapo wanafunzi huhamisha baadhi ya sifa kutoka lugha ya kwanza na kuziingiza katika lugha ya pili wanayojifundisha. Uhamishaji wa yaliyosomwa, mbinu za mawasiliano katika lugha lengwa na ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa pia ni sababu nyingine tulizozitambua kwamba huenda zilisababisha kutokea kwa athari hizo. Vilevile tumetumia kielelezo cha mchoro wa mviringo wa asilimia ili kuonyesha viwango vya athari hizo katika insha za Kiswahili sanifu za wanafunzi tuliowachunguza.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tunashughulikia muhtasari ambapo tunapitia yaliyomo katika kila sura kwa ufupi, matokeo ya utafiti tulioufanya, mahitimisho yetu kwa kurejelea madhumuni ya utafiti na mwishowe tumependekeza utafiti zaidi unaohitajika.

### 5.2 Muhtasari

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia masuala ya kijumla kama vile: utangulizi, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti huu, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

Katika sura ya pili tumeshughulikia ubainishaji na uainishaji wa fonimu za Kiswahili sanifu pamoja na fonimu za lahaja za Kiamu na Kitikuu. Katika kufanya hivyo tulibainisha fonimu za konsonanti na za irabu kwa kupambanua sifa za lahaja hizi na kuziwasilisha katika majedwali mbalimbali. Kila mojawapo ya lahaja hizi ilijitokeza kuwa na idadi tofauti ya fonimu hasa za konsonanti ingawa tulitambua kwamba nyingi ya fonimu za konsonanti kati ya lahaja hizi zinafanana tofauti inayojitokeza ni kwa kiwango kidogo. Fonimu za irabu katika lahaja zote zilikuwa zinafanana katika lahaja ya Kiswahili sanifu, Kiamu na Kitikuu.

Katika sura ya tatu tumeshughulikia athari za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kiamu. Tumeonyesha mifano ya baadhi ya maneno katika lahaja ya Kiamu na vilevile kuonyesha maneno hayo yanavyopaswa kutamkwa au kuandikwa katika Kiswahili sanifu. Pia tumeonyesha athari mbalimbali za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na athari ya lahaja ya Kiamu ambapo tumeonyesha jinsi wanafunzi wanavyobadilisha sauti katika Kiswahili sanifu kutokana na mazoea ya kutumia lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kiamu. Aidha tumeelezea sababu ambazo huweza kuchangia kutokea kwa hali hizo kwa mujibu wa michakato mitano ya nadharia ya Lugha Kati. Pia tumewasilisha katika mchoro wa mviringo ili kuonyesha asilimia ya wanafunzi tuliowachunguza na kudhihirisha kuwa na athari hizo au kutokuwa na athari hizo tulizozitambua.

Katika sura ya nne tumeshughulikia athari za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kitikuu ambapo tumeonyesha athari mbalimbali zinazojitokeza katika Kiswahili sanifu wakati

wanafunzi wanabadilisha sauti moja kwa nyingine kutokana na uzoefu wao wa kuzungumza lugha ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kitikuu. Pia tumeonyesha mifano ya baadhi ya maneno katika lahaja ya Kitikuu na kuyaandika maneno hayo katika Kiswahili sanifu. Aidha tumeelezea sababu ambazo huenda zilichangia kutokea kwa hali hizo kwa kurejelea michakato ya nadharia ya Lugha Kati kama tulivyoijadili hapo awali. Pia tumewasilisha katika mchoro wa asilimia ya wanafunzi waliokuwa au kutokuwa na kila mojawapo ya athari tulizozibainisha.

### 5.3 Matokeo

Imejitokeza kuwa lahaja ya Kiamu ina aina mbalimbali za fonimu. Fonimu za lahaja hii ni za aina mbili kuu yaani za konsonanti na irabu. Tulitambua kwamba fonimu za konsonanti za lahaja ya Kiamu zimegawika katika makundi sita makuu na pia kuna fonimu mbili za nusu irabu au viyeyusho. Pia tuligundua kwamba lahaja ya Kiamu ina irabu tano ambapo kuna irabu za mbele, nyuma, chini na kati. Kwa jumla tuligundua kuwa lahaja ya Kiamu ina konsonanti ishirini na nane, viyeyusho viwili na irabu tano. Hivyo kutokana na hili tuliweza kufikia lengo letu la kwanza katika utafiti wetu.

Tuliweza kutambua kwamba lahaja ya Kitikuu ina aina mbili kuu za sauti. Sauti za konsonanti na irabu ambapo tuligundua kwamba sauti za konsonanti za lahaja ya Kitikuu zimegawika katika makundi sita makuu na pia kuna viyeyusho viwili. Vilevile tulitambua kwamba lahaja ya Kitikuu ina irabu tano ambapo kuna irabu za mbele, nyuma, kati na chini. Kwa jumla tuliweza kubainisha kuwa lahaja ya Kitikuu ina konsonanti ishirini na saba, viyeyusho viwili na irabu tano. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa tuliweza kufikia lengo letu la pili katika utafiti wetu.

Idadi kamili ya fonimu za Kiswahili sanifu limekuwa suala lenye utata kwani wataalam mbalimbali wana maoni tofauti tofauti kuhusiana na idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili sanifu. Tuliweza kujadili maoni mbalimbali ya wataalam kuhusiana na maoni yao kuhusu idadi ya fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu. Katika utafiti wetu tulichukua mwelekeo wa uainishaji wa fonimu za Kiswahili sanifu wa Iribemwangi (2010) ambapo tuliorodhesha kwamba konsonanti za Kiswahili sanifu zimegawika katika makundi sita makuu, viyeyusho viwili na irabu tano. Kwa jumla tuliorodhesha kwamba Kiswahili sanifu kina konsonanti ishirini na tano ,

viyeyusho viwili na irabu tano. Kutokana na maelezo haya ni wazi kwamba tuliweza kufikia lengo letu la tatu katika utafiti wetu.

Imebainika kwamba, lahaja ya Kiamu ina athari katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Hili lilijitokeza wazi katika insha za Kiswahili sanifu za wanafunzi tuliowachunguza ambapo tuligundua kwamba kutokana na uzoefu wao wa kuzungumza lugha yao ya kwanza ambayo ni lahaja ya Kiamu, wanafunzi hao walihamisha baadhi ya sifa fulani kutoka lugha yao ya kwanza na kuziingiza katika Kiswahili sanifu na hili lilisababisha kuibuka kwa miundo ya maneno isiyokubalika katika Kiswahili sanifu na kuchukuliwa kuwa ni makosa. Tulitambua kuwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kiamu hubadilisha baadhi ya sauti za maneno ya Kiswahili sanifu na kuchopeka sauti wanazozitumia katika lugha yao ya kwanza kama tulivyoonyesha katika mifano ya maneno. Kutokana na maelezo haya ni bayana kwamba tuliweza kufikia lengo letu la nne katika utafiti wetu kwani tuliweza kuonyesha athari hizi za kisauti katika Kiswahili sanifu.

Ilidhihirika kwamba lahaja ya Kitikuu ilikuwa na athari miongoni mwa wanafunzi wanaojifundisha Kiswahili sanifu. Hili lilibainika katika kazi andishi za wanafunzi tuliowachunguza ambao lahaja ya Kitikuu ndio lugha yao ya kwanza kwani tulitambua kuwa baadhi ya wanafunzi walikuwa wanabadilisha sauti katika maneno ya Kiswahili sanifu na kutumia sauti wanazozitumia katika lugha yao ya kwanza. Hili lilisababisha kuibuka kwa miundo isiyokubalika katika Kiswahili sanifu na kuchukuliwa kuwa ni makosa. Kwa kuchunguza makosa hayo, imekuwa wazi kwamba wanafunzi hawa wanafanya makosa hayo kwa sababu ya kuhamisha mifumo ya kiisimu ya lugha yao ya kwanza na kulazimisha mifumo hiyo katika kujifunza Kiswahili sanifu. Badala yake wanaishia kufanya makosa hayo na kuibuka na lugha kati. Kutokana na maelezo haya ni bayana kuwa lengo letu la tano limetimizwa kwani tuliweza kuonyesha kwamba kulikuwepo na athari za kisauti katika Kiswahili sanifu kutokana na lahaja ya Kitikuu.

Katika utafiti wetu tulitambua kwamba lahaja ya Kiamu na lahaja ya Kitikuu ni lahaja ambazo zilionekana kuwa na mfanano mkubwa katika fonimu za kila mojawapo ya lahaja hizi. Zaidi ya hayo lahaja hizi zilikuwa na baadhi ya athari za kisauti zilizofanana katika matumizi ya

Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza. Miongoni mwa athari tulizozitambua kwamba zinafanana katika lahaja hizi mbili ni kama vile: matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/, matumizi ya /t/ badala ya /tʃ/, matumizi ya /d/ badala ya /ɟ/ na udondoshaji wa /l/ katika maneno ya Kiswahili sanifu. Hata hivyo tulibainisha kwamba athari ya matumizi ya /z/ badala ya /v/ ilijitokeza tu miongoni mwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kiamu katika matumizi yao ya Kiswahili sanifu.

Aidha tulitambua kwamba lahaja ya Kitikuu ilikuwa na athari katika Kiswahili sanifu ambazo zilidhihirika tu miongoni mwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kitikuu. Miongoni mwa athari hizi za kisauti ni kama vile: matumizi ya /ð/ badala ya /z/, matumizi ya /v/ badala ya /w/, matumizi ya /ð/ badala ya /v/ au /vy/, matumizi ya /n/ badala ya /m/, matumizi ya /n/ badala ya /ɲ/ na udondoshaji wa /m/ na /j/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Katika utafiti wetu tulibainisha kwamba athari hizi zilijitokeza tu miongoni mwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni lahaja ya Kitikuu tuliowachunguza.

## 5.4 Hitimisho

Tulitambua kwamba lahaja za Kiamu na Kitikuu ni lahaja zinazofanana kwa kiwango kikubwa kwani nyingi ya fonimu tulizozibainisha za lahaja hizi zilikuwa zinafanana na nyingi ya athari za kisauti tulizozitambua zilijitokeza katika lahaja hizi mbili.

Kutokana na utafiti wetu ilibainika kuwa lahaja za Kiamu na Kitikuu zilikuwa na athari mbalimbali katika matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambapo athari ya matumizi ya /j/ badala ya /ɟ/ ilionekana kudhihirika kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza ambao ni wazungumzaji asilia wa aidha lahaja ya Kiamu au Kitikuu. Katika lahaja ya Kitikuu tuligundua kuwa athari katika matumizi ya /n/ badala ya /m/ ilijitokeza kwa kiwango kikubwa sana miongoni mwa wanafunzi tuliowachunguza. Hivyo ni muhimu kwa walimu wanaofunza lugha waelewe ni makosa yepi yanayotokea kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanafunzi ili watumie mbinu zifaazo za ufunzaji wa fonolojia ili kupunguza makosa hayo.

### 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu hauwezi kudai kwamba umeshughulikia athari za kifonolojia za lahaja za Kiamu na Kitikuu katika matumizi ya Kiswahili sanifu kikamilifu bali ni matumaini yetu kwamba tafiti nyingine zitaweza kutalii masuala haya na mengine kama vile ulinganishi na ulinganuzi wa miundo ya silabi za Kiswahili sanifu na lahaja za Kiamu na Kitikuu.

Utafiti zaidi ufanywe kuhusu ulinganishi wa nomino ngeli za lahaja za Kiamu na Kitikuu na Kiswahili sanifu

Ni matumaini yetu kwamba walimu wa shule zinazopatikana katika maeneo ambapo lahaja za Kiamu na Kitikuu huzungumzwa kama lugha za kwanza watatilia maanani mafundisho ya fonimu kamili za Kiswahili sanifu katika madarasa yote ili kuweka msingi thabiti wa matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi ili kuweza kujiepusha na makosa kama yale yaliyodhihirika katika insha za wanafunzi tuliowachunguza.

## MAREJELEO


Bakari, M. (1982) The Morphophonology of Kenyan Swahili Dialects, Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chepkwony.J. (1993) Makosa Yanayofanywa na Baadhi ya Wanandi Katika Matumizi ya Kiswahili , Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chiraghdin na Mnyampala (1977) *Historia ya Kiswahili*, Nairobi : Oxford University Press.

Chomsky, N na Morris, H (1968) *The Sound Pattern of English*, New York: Harper & Row.

Corder, S. (1967) *Error Analysis and Interlanguage*, Oxford: Oxford University Press.

Ellis, R. (1989) *Understanding Second Language Acquisition,* Oxford: Oxford University Press.

Habwe na Karanja (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili sanifu,* Nairobi: Phoenix Publishers.

Iribemwangi, P. (2010) *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*, Saarbruken: Verlag.

Iribemwangi, P. na Mukhwana, A. (2011) *Isimujamii*, Nairobi: Focus Publishers.

Khansir, A. (2012) *Theory and Practice in Language Studies,* Finland: Academy Publishers.

Kihore, Y., Massamba, D. na Matangila, M. (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu,* Dar es Salaam: TUKI.

Larsen, D. et al. (1992) *An introduction to Second Language Acquisition Research*, London: Longman.

Massamba, D., Kihore, Y. na Msanjila, Y.(2004) *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu,* Dar es Salaam: TUKI.

Maundu , M. P. (1980) Sound Change and the Reconstruction of Kikamba Consonant Sounds in Natural Generative Framework, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbula, J. (2011) Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia Yanayofanywa na Wazungumzaji wa Kikamba Wanapojifunza Kiswahili Sanifu, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mgullu, R. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili,* Nairobi: Longhorn.

Mutahi, K. (1977) Sound Change and the Classification of the Dialects of Southern Mt. Kenya, Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu et al. (2006) *Sarufi ya Kiswahili : Uchanganuzi na Matumizi,* Nairobi : JKF.

Otiende, A. (2013) Athari za Kimofofonolojia za Kiolusuba Katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu kama Lugha ya pili, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Polome,(1967) *A Handbook of Swahili Language,* Nairobi: Jomo Kenyatta Publishers.

Rapando, M. (2005) Makosa ya Kimofo-sintaksia Yanayojitokeza Katika Kazi za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Rustipa, K. (2011) Contrastive Analysis, Error Analysis, Interlanguage and the Implication to Language Teaching, *Language and Linguistics.* Ragam Jurnal Pengembangan Humaniora, vol.1

Selinker, L. (1992) *Rediscovering Interlanguage*, London: Longman.

Tarone, E. et al. (1976) *Systemacity/Variability and Stability/Instability in Interlanguage System*, Michigan: University of Michigan Press.

Tarone, E. (2006) *Interlanguage.* United Kingdom: Elsevier ltd.

KIAMBATISHI A: KIAMU

Swaleh Babu Swaleh Shee

Lamu Boys pri schooll

Class seven (7)

SIKU AMBAYO SITAISAHAU MAISHANI

Ilikuwa siku ya sabato, mimi na sahibu zangu tulikuwa tumeingojea kwa hamu na ghamu. Kutwa kucha kina nyoko walinena siku hiyo. Hatimaye iliwadia. Ilikuwa siku ya karakala za tamaduni za Amu.

Zijana ziliazana furifuri, wakongwe walikuwa ndi sihaba, kushashua siku hiyo. Kulikuwa na mashindano mbalimbali, simajahazi, siupishi, si punda, si densi, si kutoma, sikuogelea na menginezo.

Watalii kutoka kila pembezoni ya dunia waliyazana, kujionea fahari mji wetu wa Amu. Pundesi punde mashindano ya punda yalitia habta. Ama kweli ukiona za elea yua zimeundwa.

Mda wa jibwa kuukelia mkiawe, mbio ziliti puka. Kulikua na upinzani licha ya hayo asiye kubali kushindwa simshindani. Punda kwa ina la chukuzee alitimuka mkukimkuki mithili ya pikipiki za olimpiki.

Kisha hapo insi kutoka ajo wilingia bandarini Mashua kwa ina la Uhunuto ndio ilipata nswi boko mwenye takribani kilo thaini. Ndio maana wavuvi waliamba kuwa mwenda ago hanyeli henda kawia papo.

Baadaye tuliende kuyana mapishi kwa kina nina na mabanati. Zakula hizo zilikuwa sherubati za kunazi, sambusa za samaki, biriani ya mayai ya ndiwa, zlazi za mbati na zingi zenginezo.

Watu weng walingojea kwa hamu mashindano ya kuogeleya kulikuwa na zijana mahiri walobombeya kwenye kuoga. Shindano hilo

LAMU PRIMARY S. 7NORTH

MBARAK AHMED OMAR

SIKU AMBAYO SITAISAHAU

Nilipomaliza kusoma masomo yangu ya darasa la nane, Wazazi hawakuwa na pesa za kunipelekea kumaliza masomo yangu. Kwa bahati mzuri nikapata kibarua kwenye uwanda wa ndege.

Nilifurahi kwa sababu nikawa hakuna ndia nyingine ya kupeleka maisha. Siku ikafika nakuanda kazi. Siku zikapita nazo miaka ikapita. Mara siku moja nilipokuwa kwenye ndrege nasafisha nikaona kibuku cha zungumzia maelezo namna ya kurupeka ndege.

Kwa udarai na pupa nilizokuwa nazo, niitaanda kujaribu kupeleka huku nikijimakini najua kila kitu baada ya maagizo yale. Kaketi kitini bila wasiwasi. niliandda na kubonyeza kibonyenzo cha kwanda, nikaona banka likaanza kuringa, nikabofd cha pili, nikaona yendao, kabonye-za cha tatu ikaanda kupaayuu na huku ikiendelea kuenda.

Niliporudi kwenye kibuku cha maagizo, kilikuwa kimefika mwisho. nikaanza kutokwa na jasho, Mamangu mzazi macho yalinitoka. Nilikuwa siyuila kutenda kwenda siwezi kurudi balad.

Kwa bahati nzuri nikasikia sauti ikiniambiya. Namna ya kuteremsha ndrege yalikuwa maigizo marefu, Nilikuwa mtiifu na mwenye kufuata hayo maigizo yao hadi nikasikilia tini.

Nikashuka salama salimini huku roho ikiniendam mbiyo. Nilipofungua mlango wa

KIAMBATISHI A: KIAMU

# SIKU AMBAO SITAISAHAU

Daima dawamu, sikuwa nimeyuia maana ya chochote king'aacho si dhahabu. Kisa kimoya ndicho kilinifundisha adabu. Kilinifanya niyue maana ya methali hii na kunipa mafunzo kemkem. Nisingeona bashasha mya mwengine akianguka kwa mateso yaliyonipata.

Ilikua siku ya Juma tano, nilipoamka nikiwa mzima kama kigongo. Nilizinduka miali ya yua ilipokua ikichomoza kwenye dirisha letu. Nilipoamka tu, niliyua bayana siku hiyo ingekuwa ya kumbukumbu. Naam, siku njema huonekana asubuhi.

Baada ya mlo umeandaliwa na mama, mama yangu alinipasha habari. Aliniyulisha kuwa yeye na baba yangu wangekwenda sokoni siku hiyo. Wangeniyata nyumbani peke yangu. Mimi kusikia hivyo, nilishikwa na wasiwasi wo mwasi. Sikuwahi kukaa peke yangu maisha yangu. Mamangu kuona hivyo, alijaribu kunibembeleza akisema ningekuwa sawasawa. Alinipatia nasaha. Aliniambia nisimfungulie mtu yeyote mlango.

Hata akinifanyaye nisimfungulie mlango katu. Sikutia nta masikione na nilimsikia kwa makini. Baada ya hao, alikwenda pa mtima pa moyo hadi sokoni. Basi ikawa mimi na nyumba yetu. Niliketi kitako nikiangalia vipindi kwa raha mustarehe

KIAMBATISHI A: KIAMU

LAMU PRIMARY SCHOOL.

SIKU AMBAYO SITAISAHAU.

Siku hiyo ilikuwa ni siku ya ndoa kunla mwanae Kwani siku hiyo tuliiyongoja kwa hamu na hamumu ilikuwa ni siku ya harusi ya kaza ni yangu.

Tulisafiri na kwendra Mambasa katika harusi. Tulipofika Mambasa tulikuwa tumechoka sana kwa matoju ya gari. Basi tuliingia chumba cha wageni na kwendra kupunzika.

Baada ya masaa katiti tulishuka tini na kwendra kufanya kazi na hata kutayarisha chakula mbalimbali kama vile ziaai za kukangwa, matobosha, sambusa na zengine zo zifuatazo.

Na hata pia tuliendra sokoni na kununua zitunguu, tomato, pilipili, kiangopepeta na pilipili duka. Tulipotoka sokoni tuliendra dukani na kupimisha ziatu, kisha tukarudi nyumbani!

Tulipofika nyumbani ilikuwa ni ala siri. Na kuanda kuipamba. Na mimi sikubakia nyuma nikaitayarishia. Nilipomaliza tuliendra holini. Kuipambwa na kukawa kuzuri sana.

Watu wote walikatika kiuno mpaka wakanena basi hata nami sikubakia nyuma nilikatika kiuno kama mwandaimu niliorukwa.

Mara naye Mwanamuziki "DJ" akasimamisha nyimbo na kutukuwa spika na kunena hiyau kwamba biharusi ataka kungia kwenye holi na kuketi kwenye sitafi.

KIAMBATISHI A: KIAMU

Stid 7

Lamu boys Primary School

HAITHAM MZEE BW. MKUU

SIKU AMBAYO SITAWAHI ISAHAU

Ilikuwa asubuhi na mapema mama yangu alikuya kuniansha ilikuwa ni siku ya safiri. Ilikuwa safiri yakuelekea Nairobi nakuona zitu za ajabu.

Safari alianda saa mbili na mapema na kuanda na safari. Mara nikaona majumba makubwa makubwa huko Nairobi kisha tukaenda nyumbani na tukapokewa kwa mikono miwili.

Kulikuwa na harusi ya kukata na shoka ilikuwa ni harusi ya anti yangu wa Nairobi. Mara tukawaona watu wanaingia kwa wingi mara sisi tushuke tini sherehe inaanda.

Mara bw. harusi aliitambulisha kwa watu mara ikaekwa nyimbo na watu walianda kuteza kila mmoja wao walikuwa na mke wake. watu waliteza mpaka wakachoka.

Kisha ilifika muda wa chakula watu wote waliambiwa waketi tini ili wapata kutiliwa chakula watu walipomaliza kula waliambiwa kila mmoya aende kuitaarisha kwa sababu ulikuwani wakati na kupija picha na bwana na bibi harusi.

Baada ya muda mfupi insi walianda kushuka tini walikuwa wameshaitaarisha walivaa nguo nzuri na ya kuvutia. Mara wakaambia kila mmoya aende jukwaani.

Akafika ni muda wa mamangu na babangu kupija picha na bwana na bibi harusi baada ya wao kupija picha ukafika ni muda wa kula chakula cha usiku watu wote waliketi kwenye meza walianda kupakuliwa chakula na wakala bila shida yoyote.

KIAMBATISHI B: KITIKUU

MATESO YA MAMA WA KAMBO.

JINA LA MWANAFUNZI. THUREYA ABUUBakar.

SHULE NA DARASA. Shule ya msingi ya wasichana faza.

MJI NA COUNTY. mji wa faza County ya lamu.

Mame wa kambo ni mame ambae babangu alimuovoa. na ni mame ambae hakunidhaa. bali alimuovoa kwa madhumuni fulani. Kama kuvaea vana alivovapacha kwa nke aliechangulia kumuovoa.

Lakini huu mame wa kambo iye havatukulii vana hava-kama vanave. Lakini hutegemea na mama uliempacha baada ya babako au babangu kuovoa bahati ikiva nduri wawedha kumpacha ~~mama~~ wa kambo akakupe ndae na kukutukulia kama mwanawe aliendha kwa machumbo ake.

Pio kuna mama vangine havana hikima wala busara ivo huvatukulio vana havo kama maadui vake hio huwa si tabia nduri kwa bwanadamu hata dini echu akisilamu huchwambia tuvasaidie valee ambavo mmayatima ama valee ambavo pvanda honwa na vadhadhi vavo.

Nchu hutanja ghera kachika mambo kama hao mwana aketie na mamake wa kambo hutegemea vangine huketi na vo kudhuri lakini vangine huva na roho kavu nno hafikirii kama kuna vake na vandue iye kadhi hufikiria vake. Vana vangine hupacha machteso makuru kama havaketi na vadhadhi vake alivovadhaa.

Haa ni machteso ambao mwana akiketi na mamake wa kambo huuapacha. kama kutompa kula mwana aketie na mama wa kambo ambae hampendi amahantukulii kama mwanae huva hapawi kula. pili ni nguvo pia nguvo hampi mfano siku aidi vana huvaa vauee nguvo nduri cia ule aketio na mamake wa kambo na ul

KIAMBATISHI B: KITIKUU

MAISHA YA VIJIJINI

JINA LA MWANAFUNZI Ruhkiya Said.

SHULE NA DARASA Shule ya msingi ya wasichana / 7

MJI NA COUNTY Bajini / FAZA Lamu

Maisha ya vijijini ni magumu mno. mwanzo kijijini hakuna taa kisha vachu huvaza dhibahalulu. kisha vachu va dhijijini ni masiki ni pia kupacha kula huvona nitabu kwavo. Hoko dhijijini hakuna sikuli wala chuvo. dhijiji ni huvona kuna vanyama vahatari mno. kama hiya noka, simba, pisi na vanyama vangine.

Kuketi kijijini huva wenzao hanzu nno usiku hupachi kuyala kwasababu ukisikia chuvo huvona vidhi vantha ngia. Asubui ukinyuka huvona mpaka unende inthe ukanae ama kuosa vuso. dhijijini huvona ntabu sana kupacha maji akunwa ukitaka maraku nwa mpaka unende iyini. Na ukitaka kufanya biashara huvona mpaka unende inyini kudhanya dhichu pia huvona nakuna dhichu dha dukani.

Kuketi dhijijini mpaka asubui na mapema unende sikuli hoko sikuli kwenyewe huvona mbali na ukichelewa sikuli huvona hupondwa na ukitoka sikuli huvona hunenda chuvoni mpaka choruchipo minadhini huvona ni usiku na ambapo hoko minadhini hakuna taa ńka ndili. hidhokandu dhenyewe huvona ni mararuko. Mwanadamu hunenda sikuli bila dhiachu. Na ikisikilia siku aidi huvona huna kandu dha idi. hao mapeni huvona ntabu kupacha. Ukinenda iyini kudhanya dhichu sangine huvona dhich hadhinu nuliwi chochote ukirudi hurudi na ipeni

KIAMBATISHI B: KITIKUU

TWAHA ABDALLA

Siku ni Siyoweza Kuisahau!

JINA LA MWANAFUNZI, TWAHA ABDALLA

SHULE NA DARASA. SHULE YA FAZA DARASA LA SABA.

MJI NA COUNTY, faza na lamu.

Siku moya chulikwenda minadhini imi na marafiki dhangu. chuliposikilia minadhini kulikuva kete sana. Isi chulishidwa kuiva kuva kundatokea kichu gani?

Siku hiyo ulikuva ni siku dha dhichakwi. Niliyambia marafiki dhangu hakuna kichu chochote toani dhikapu chuchieni dhichakwi.

chulipoumalidha mchakwi wa kwanda chuliyenda mchakwi wa pili ulikuva na dhichakwi dhingi ndo. chulipa uyadha mfuko kwanda chukautoa mfuko wa pili.

chukaanda kutafuta mchakwi ngine. chulipouyona chuliyona una dhingi kuiliko michakwi ya mwando. chulipousongelea mbele chulisikia mvumo kwa mbali.

Chuliposikila karibu dhaidi chulisikia sauti ya mvumo kwa ukuu dhaidi, ania nawedha kunena iliyali ka kama radi.

Chuliachuka na chukaanda kukimbio chulipoangalia mbee chukamuona fisi mkuru sana. Imi na rafiki dhangu hachukujua chufanyeye wa chuchendeye.

Imi kavambia angikani dhisimbo iyu dha kitwa. Chulipoangika dhisimbo dhitwani iye hakukiri. Imi katoa ishembee langu nikavambia rafiki dhangu kitini nima angu.

KIAMBATISHI B: KITIKUU

SIKU AMBAYO SITOWEZA KUISAHAU

JINA LA MWANAFUNZI Msellem Moh'd Msellem

SHULE NA DARASA FAZA BOYS STD 7

MJI NA COUNTY FAZA LAMU

Siku moja ramadhani chulikwenda nsikichini kufanya mashindano akusoma kuruani mara chulisikia vachu vakibika kele mocho! Mocho!

Hachukupotedha hataa sekunde moja chulitoka kama mibudhi amadikale ikitolewa kidhidhini. Chulikuva chukipandana iyyu kwa iyyu.

Ilikuva ni siku ya juma ntana, chulipotoka vanavadoda valiambiwa vakimbilie pwani kwa sukuli. Nilikuva nnene lakini nlivapicha vachu vote kwa mbio hata mahodari vambio nlivashinda.

Chulipo sikilia nilinvona rafiki angu akinlilia ishe na inya so vakavaka kisha vakokeka kama minofu a mbudhi.

Lakini vachu vavuli valinenda kuudhima mocho. Mocho ulipodhima chulirudi nnyjini ndiani chulivavona kuku, dhichumbo dhindapasuka.

Niliponenda numbani nliivona numba echu haikudarwa na mocho wala uharara wake. Ilikuva ni siku ambo siwedhi kuisahau

Faza road Nairobi

KIAMBATISHI B: KITIKUU

YALIO NI HUSU KUMSAIDIA MAMA

JINA LA MWANAFUNZI YAYE Abdalla

SHULE NA DARASA Shule ya msingi ya wasichana / Darasa La Sabo

MJI NA COUNTY Rasini / Faza

Siku moya nilimdinka mwana mmoya husaidia mya na mamake nae hawedhi ana baridi. Sasa imi kapita nilipo muona ule mwana nami kasikia kwamba nami hufaa kunsaidia mame nami ni pache radhi kwa mame ili nami nisaidike duniani nami. niliudi numbani mbio kwa furaha dhangu ili nami nisaidiye mame. Mame akanambia amwanangu we mbona undakuya mbio. Mame imi nataka kusaidia hapa numbani ili nami nipendeke hapa numbani.

Siku apili mame alina mbia imi ili imi nimpi kie. sikunungunika achi sitaki kupika kamambia mame anipe dhichu dhakupikia. Babangu alipokuya akanambia amwanangu shika hau isi udasanye nasi chupache kula toka na asubuhi hachuyala. hiya nkwambiauo mwanangu isi hachu kupacha sinti dha kachumbi. Hiya nkwambiauo chwataka kwenda tena kusu cha yuwa. Sasa mwangu uwe nsaidie nyawe kesho nkupeke sikuli nawe usome. Sawa baba. mame weche hauo isi muasanye na sichule. Baba aliporudi Baha rini. Sasa mame hufanya dhiadhi sakumi sasa imi husaidi name ili nami nisaidike.

ukimsaidia nyawe hupacha dhawabu kwa mungu kwa nyawe hukosi heri yoyote. Kuna siku ngine mame alikuva hawedhi. Sikukwenda sikuli nikava hunshughulikia iye kimpa mai na kula showe akia upe kula na ungineuo,